# Utangulizi

Mkakati wa Kupunguza Umasikini (MKU) ni 'sera mama' ya nchi. Kusudio lake kuu ni kuweka kipaumbele kwenye hatua zinazopunguza umasikini, kuinua ubora wa maisha na ustawi wa watu masikini na kuleta hali ya kutenda haki na kuheshimu haki za binadamu. Sera nyingine zote na bajeti zinatakiwa kwenda sambamba na MKU.

Kipindi cha utekelezaji wa MKU wa sasa kimemalizika. Hivi sasa Serikali inaandaa Mkakati mpya wa Kupunguza Umasikini (MKU II) utakaotoa mwongozo kwa nchi yetu katika kipindi cha miaka mitano ijayo kuanzia 2005 hadi 2010. Maandalizi ya mkakati huu yamefanyika kwa kuzingatia tafiti nyingi za uchambuzi na maoni kutoka kwa wananchi. Hivi sasa rasimu ya kwanza ya MKU II imekamilika. Serikali ingependa kupata maoni maalumu kutoka kwa wananchi kuhusu namna ya kuiboresha rasimu hii.

NGO Policy Forum (NPF) – ni muungano wa Asasi zaidi ya 70 Zisizo za Kiserikali (AZISE) zinazojihusisha na michakato ya sera kwa lengo la kuwezesha ushiriki mkubwa zaidi wa umma katika michakato hiyo. Tumetayarisha chapisho hili na kulisambaza sehemu zote za Tanzania ili kuwawezesha wananchi kupata taarifa, kujadili rasimu ya mkakati mpya na kutoa maoni yao.

Waraka huu ni **muhtasari usio rasmi** wa vipengele muhimu vya rasimu ya MKU II. Umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inatoa muhtasari wa Muundo wa MKU unaopendekezwa, ukijumuisha misingi yake mikuu. MKU unalenga katika kupunguza umasikini katika maeneo makuu matatu ambayo ni: kuongeza ukuaji wa uchumi; kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na kuimarisha utawala bora na uwajibikaji. Sehemu ya pili inawasilisha malengo makuu, matokeo tarajiwa na mikakati ya utekelezaji katika kila eneo, kati ya maeneo hayo matatu.

**Unaweza kufanya nini?** Unaweza kusoma rasimu hii na kuelewa ni nini Serikali inapanga kufanya. Jadili na rafiki zako, majirani na hata wafanyakazi wenzako. Iwapo utakuwa na maoni mahsusi ya kuiboresha – kama vile kuangaliwa upya kwa jambo lolote ambalo tayari limo katika rasimu hii, au kuongeza jambo jingine muhimu ambalo limesahaulika –usisite kuyatuma kupitia AZISE zilizo karibu yako kwa anuani ifuatayo: Mapitio ya Mkakati wa Kupunguza Umasikini, Ofisi ya Makamu wa Rais, Kitengo cha Kuondoa Umasikini, SLP 5380, Dar es Salaam. Maoni yawe mafupi na yalenge katika suala mahsusi. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maoni yako ni tarehe **10 Septemba, 2004.**

Iwapo hautapenda kutoa maoni yako, au utakuwa umechelewa kufanya hivyo, bado utaweza kutumia waraka huu kwa taarifa, majadiliano na midahalo. Ukiwa kama mwananchi una haki ya kufahamu kuhusu sera na kujadili masuala hayo katika jamii yako. Pia utaweza kulinganisha rasimu hii na ya mkakati unaotarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.

**Sera ni kuhusu watu.** Sote tuna nia ya kuufanya MKU II kuwa ni mkakati utakaowahudumia kwa dhati wananchi wa Tanzania. Fanya kile unachoweza kufanya leo ili kuleta mabadiliko!

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:
Sekretarieti
NGO Policy Forum (NPF)
S.L.P.38486 Dar es Salaam
Simu/Faksi: +255 22 2121288
Barua pepe: npf@cats-net.com or prs@cats-net.com




Seri K. anasema...
HAYA YAMEPITWA NA WAKATI ... TUNATAKA MKAKATI WA WATANZANIA WENYEWE


# Muundo wa MKU II
# (Mkakati wa Pili wa Kupunguza Umasikini)

Umasikini una sura na vipengele vingi. Unayagusa makundi mbalimbali ya kijamii na hata mikoa na maeneo mbalimbali kijiografia kwa njia tofauti. Ili kuuelezea umasikini kikamilifu, ni lazima ukusanye taarifa kwa njia mbalimbali na kutoka katika makundi tofauti ya kijamii. Hii ndio sababu Mkakati Mpya wa Kupunguza Umasikini (MKU II), unatumia takwimu kutoka katika vyanzo vikuu vitatu ambavyo ni; maoni ya wadau mbalimbali yaliyokusanywa katika mlolongo wa mashauriano, matokeo ya tafiti zilizofanyika hivi karibuni na uzoefu na mafunzo yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mkakati wa mwanzo.

MKU wa kwanza ulitekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu, 2000/01 – 2002/03 na ulilenga katika sekta za kipaumbele. MKU II utatekelezwa katika kipindi cha miaka mitano, 2005/6 – 2009/10. Mkakati huu mpya unaweka msisitizo zaidi katika kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, hivyo ni mkakati ambao mbinu yake kuu ni kuelekeza jitihada katika kufikiwa kwa matokeo yaliyoainishwa (outcome-oriented). Mkakati unalenga kuziunganisha sekta mbalimbali ili kushirikiana pamoja katika kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Malengo Makuu katika Kupunguza Umasikini**

MKU II unalenga katika matokeo ya utekelezaji wa sera na shughuli zinazokusudiwa kupunguza umasikini. Matokeo hayo yamewekwa katika maeneo makuu matatu: (1) Ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; (2) Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na (3) Utawala bora na Uwajibikaji . Matokeo haya matatu yanategemeana, huku kila moja likisaidia na kuimarisha utekelezaji wa jingine kama inavyoonyeshwa katika kielelezo kifuatacho:




**1: Ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato**

Sifa nne za ukuaji wa uchumi ambazo ni muhimu katika kupunguza umasikini ni:

*Kwanza, ni lazima ukuaji huo uwe ni ule unaowagusa watu wengi na kwa usawa.* Sera na hatua maalumu zinahitajika ili kuelekeza rasilimali kwa makundi ya jamii katika sehemu za nchi au sekta zilizo masikini zaidi ili kuziwezesha kushiriki katika shughuli za uzalishaji au katika utoaji wa huduma za jamii. Ni lazima kutoa msaada wa kutosha na kujenga mazingira mazuri yatakayowezesha matumizi mazuri ya rasilimali hizo.

*Pili, ukuaji lazima uwe mkubwa na endelevu*. Hii inamaanisha kuwa ni lazima nchi izalishe viwango vikubwa na endelevu vya akiba ya ndani na uwekezaji. Pale inapobidi kutafuta misaada kutoka nje, basi ni lazima misaada hiyo itumike kwa busara na uangalifu ili iweze kuiweka nchi katika mwelekeo thabiti wa ukuaji. Ni lazima nchi ihakikishe kuwa shughuli za maendeleo za kizazi cha sasa haziathiri mahitaji ya maendeleo ya kizazi cha kesho. MKU II unatambua haja ya kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za nchi na kuepuka athari mbaya kwa mazingira.

*Tatu, mkakati wa ukuaji ni lazima ujumuishe mkakati wa biashara.* MKU II utazingatia na kutekeleza Sera ya Taifa ya Biashara na kuimarisha uwezo wa ubunifu na ushindani wa wazalishaji wa ndani. Mipango ya maendeleo ya biashara italenga kupanua wigo wa masoko ya nje kwa kuhimiza na kuchochea shughuli za kuongeza thamani za bidhaa, upatikanaji wa mitaji na uwekezaji katika shughuli za uzalishaji kwa ajili ya soko la nje na ustadi wa kushiriki katika masoko ya kanda na ya dunia yenye faida.

*Nne, msisitizo utawekwa katika kuongeza fursa za ajira.* Itakuwa ni muhimu sana kwa mkakati wa ukuaji uchumi kuangalia kwa makini mahusiano baina ya sekta mbalimbali ukiweka umuhimu wa kipekee kwa viwanda vitokanavyo na mazao ya kilimo na shughuli za uzalishaji katika maeneo ya vijijini zisizohusu kilimo. Hali kadhalika, sekta zinazokua na zinazoongoza katika kuchangia ukuaji wa uchumi kama vile utalii na uchimbaji madini zina umuhimu wa kipekee katika kupunguza umasikini. Sekta hizi zinatoa ajira ya moja kwa moja, zinapanua ujuzi wa watu na kutoa fursa mbalimbali kwa watu kujipatia riziki zao. Zaidi ya hayo, sehemu ya mapato ambayo serikali inayapata kutoka katika sekta hizi yatatumika katika kuboresha huduma za uchumi na kijamii, hivyo kuchangia katika maendeleo endelevu ya miundombinu na mtaji wa watu.

**2: Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii**

Eneo la pili linashughulikia uwezo, uhai na ustawi wa watu likilenga zaidi katika uhakika wa chakula lishe na makazi. Msingi imara wa sera ya kijamii ni muhimu katika kushughulikia hatari zinazoyakabili makundi mbalimbali ya watu kuangukia katika umasikini (vulnerability) na kutoa hifadhi ya jamii kwa makundi maalumu kama vile watoto yatima, watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, watu wenye ulemavu na wazee.

Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii kunategemea utoaji, uwezo wa kumudu na upatikanaji wa huduma kama vile elimu, afya, maji, matibabu na kinga dhidi ya VVU/UKIMWI na mipango ya ulinzi/hifadhi ya jamii. Zaidi ya hayo, maisha ya watu huwa bora zaidi wanapoishi katika mazingira safi na yanayolindwa; mathalan, yasiyo na uchafuzi wa hewa na maji na yasiyo na mazalia ya mbu.

Maisha bora huiwezesha jamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji ambapo wanawake na wanaume hupata fursa sawa. Vilevile tija huongezeka na kuendelezwa pale ambapo mazingira yanalindwa na kutumiwa kwa njia endelevu.

**3: Utawala na Uwajibikaji**

Eneo la tatu ndilo linaloweka msingi kwa eneo la kwanza na la pili. Ili pawe na ukuaji wa uchumi unaowagusa watu wa ngazi zote na kuimarika kwa ubora wa maisha na ustawi wa jamii ni lazima pawe na utawala bora. Suala la utawala bora linalenga katika kuangalia mifumo na michakato ya kiuchumi kama vile usimamizi wa rasilimali za umma (Fedha na maliasili), ulinzi binafsi, hali ya kuvumiliana na kushirikisha wananchi katika kufanya maamuzi, mathalan, kupitia michakato ya uboreshaji wa serikali za mitaa na kuhakikisha kuwa mifumo na taratibu za utawala ni za uwakilishi na zinazowezesha uwajibikaji wa wawakilishi kwa wale wanaowakilishwa. Mambo muhimu katika eneo hili ni haki za binadamu, mfumo wa haki na wenye ufanisi wa sheria na vita dhidi ya rushwa.

Eneo hili linabainisha amani, utulivu wa kisiasa, umoja wa kitaifa na mshikamano kama mojawapo ya malengo yake makuu. Linaweka misingi ambamo ukuaji wa uchumi na uboreshaji wa maisha na ustawi wa jamii unaweza kufanyika. Malengo mengine muhimu ni Demokrasia na uvumilivu wa kisiasa na kijamii; Utawala bora na utawala wa sheria; na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupungua kwa rushwa na wananchi kuwa na uwezo wa kupata taarifa.

Ili matokeo hayo yaweze kufikiwa ni lazima pawe na matumizi mazuri ya rasilimali yenye uwazi na uwajibikaji. Ni lazima pia pawe na mifumo na taasisi za utawala zisizo na rushwa na utawala wa umma unaofanya kazi kwa ufanisi na uadilifu. Mojawapo kati ya njia za kuongeza ufanisi ni kwa kujumuisha Programu ya Uboreshaji Huduma kwa Umma (PSRP) na Programu ya Marekebisho ya Mfumo wa Uendeshaji wa Serikali za Mitaa (LGRP) katika michakato ya Mapitio ya Matumizi ya Serikali (PER) na Mkakati wa Kupunguza Umasikini (PRS/MKU).

Vilevile, MKU II unatambua kuwa wananchi wote wana haki ya kupata taarifa zote kuhusu sera, sheria na fedha za umma. Hii ina maana kuwa ni muhimu kuboresha uwezo wa watumishi wa umma kupata taarifa zile zinazohusu sekta yao na zinazohusu sekta nyingine mbalimbali na kuboresha upashanaji habari ndani ya serikali yenyewe, ili kuwawezesha watumishi hao wa umma kushughulikia kikamilifu mahitaji ya Watanzania katika ngazi zote.

**Misingi ya MKU II**

Mkakati mpya unazingatia misingi mikuu sita ambayo ndiyo itakayoongoza sera na utendaji wake.

1. *Kwanza, mkakati huu unamilikiwa na nchi na wananchi wenyewe* na utatumika kama nyenzo ya kutekeleza ajenda ya maendeleo ya taifa.Umiliki wa nchi na wa wananchi unatokana na kuboreshwa na kuongezeka kwa kiwango cha ushirikishwaji wa wananchi na wadau wengine kwa *kupitia michakato mbalimbali ya mashauriano.* Hali kadhalika, MKU II utakuwa na mkakati wa mawasiliano ili kurahisisha uchangiaji na upashanaji wa taarifa kati ya serikali na wadau wengine.

2. Suala la usawa litazingatiwa na kushughulikiwa kikamilifu kwa kuhakikisha kuwa panakuwa na ukuaji endelevu wa uchumi unaowanufaisha wananchi walio katika ngazi zote, kuweka msisitizo katika kukuza ajira na fursa za watu masikini kujipatia riziki na kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii.


3. MKU II unaheshimu na kuzingatia kwa dhati makubaliano na mikataba ya kimataifa ya maendeleo ambayo Tanzania imeridhia, hiyo ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs), Makubaliano ya NEPAD na Mkutano wa Dunia wa Maendeleo Endelevu. Aidha, misaada ya kibiashara ambayo nchi yetu itaipata itatumika kuongeza uwezo wa wazalishaji wa humu nchini, hususan, wajasirimali wadogo wadogo na wa kati (SMEs) na wazalishaji wa vijijini ili waweze kukabiliana na changamoto za utandawazi.

4. Mkakati unazingatia kuwa umasikini na jambo pana na lenye sura na tabia tofauti tofauti.Pia unazingatia mikakati mahsusi ya maendeleo ya sekta mbalimbali, na masuala yanayogusa sekta zote (masuala mtambuko) kama vile utawala bora, mazingira, jinsia, VVU/UKIMWI, ajira, watoto, vijana, wazee na watu wenye ulemavu. Hivyo mkakati huu unagusa maeneo yote (comprehensive).

5. MKU II utatoa nafasi zaidi kwa wadau wa humu nchini, (Jumuiya huru za kiraia, sekta binafsi) katika majadiliano ya sera na kusisitizia matumizi mazuri na yenye ufanisi ya misaada katika kupunguza umasikini.

6. Mkakati unasisitiza kuendelea kuoanishwa (harmonization) kwa michakato mbalimbali ya kitaifa ya kisera, hususan, Mkakati wa Kupunguza Umasikini (PRS), Bajeti ya Serikali, Mpango wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Serikali (MTEF), Mapitio ya Matumizi ya Serikali (PER) na Mkakati wa Kuisaidia Tanzania (TAS) huku msisitizo wa kipekee ukiwekwa katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na mtiririko mzuri na unaofanyika kwa wakati wa upashanaji taarifa na takwimu miongoni mwa taasisi mbalimbali.

# Eneo la 1: Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umasikini



# Eneo 1: Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza Umasikini wa Kipato

| Tokeo Kuu Tarajiwa: |
|---|
| **Ukuaji wa uchumi unaowanufaisha wananchi wa ngazi zote kwa usawa unafikiwa na kudumishwa.** |

| Malengo | Matokeo ya kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| 1) Kuhakikisha usimamizi mzuri na wenye ufanisi wa uchumi | Dumisha uthabiti/uimara wa uchumi mpana | • Endeleza jitihada za kudhibiti mfumuko wa bei katika kiwango cha 4% kwa kutekeleza sera nzuri za fedha na kodi (dhibiti nakisi ya bajeti). | Fedha/ Kodi | Fedha, Benki Kuu |
| | | • Jitahidi kupata ziada katika mizania ya malipo ya biashara ya nje (current account of the Balance of Payment). | Fedha | Fedha, Benki Kuu,Viwanda/ Biashara |
| | | • Endeleza uthabiti wa kiwango cha ubadilishaji wa fedha (exchange rate) kwa kupitia taratibu za soko. | Fedha | Benki Kuu |
| | | • Hakikisha akiba ya fedha za kigeni inabaki katika kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa angalau kipindi kisichopungua miezi 4. | Fedha | Fedha, Benki Kuu |
| | | • Endelea kuimarisha taratibu za usimamizi wa kodi; pitia sera ya kodi na matokeo yake katika kuongeza mapato, ukuaji uchumi na ustawi wa jamii | Kodi | Fedha, TRA |
| | | • Boresha matumizi ya misaada ili iweze kuwa na manufaa zaidi kwa taifa kwa kuongeza mchango wa misaada hiyo katika bajeti na kuelekeza misaada katika mahitaji ya kipaumbele ya taifa kwa kupitia michakato ya PER na PMS. | Misaada | Mipango/ Ubinafsishaji, Fedha |
| | | • Zingatia miongozo ya uandaaji bajeti ya Kijinsia katika Mkakati wa Wizara ya fedha, shauri na endelea na jitihada za kutumia miongozo ya bajeti ya kijinsia katika sekta zote | Jinsia | Fedha, Jumuiya Huru za Kiraia |
| 2) Ukuaji wa Uchumi ulio endelevu na unaowagusa na kuwanufaisha wananchi wa ngazi zote unaendelezwa | Ongeza kasi ya ukuaji halisi wa pato la taifa hadi kufikia kiwango cha angalau 6 - 8%<br><br>Ongeza asilimia ya pato la taifa inayotokana na biashara ya nje na ongeza ushiriki wa sekta isiyo rasmi na wafanyabiashara wadogo na wa kati katika biashara (WVB).<br><br>Imarisha, endeleza na weka taratibu nzuri za maendeleo ya biashara na sekta binafsi kwa mwaka<br><br>Fikia na endeleza/kudumisha kiwango cha ukuaji wa | • Linda haki ya kumiliki mali, kupunguza urasimu na taratibu zisizo za lazima, jenga taasisi zitakazoimarisha ufanisi na ushirikishwaji wa masoko, boresha uzalishaji na tija katika viwanda, kilimo, uvuvi n.k | Utawala | Mipango Ubinafsishaji, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, OR- Ikulu, Viwanda na biashara, Sekta Binafsi |
| | | • Pitia na rekebisha sheria na mila zinazowabagua wanawake na kuwanyima haki ya kumiliki na kunufaika na rasilimali za uzalishaji na mali, sheria kama Sheria ya Mirathi, Sheria ya Ndoa inayowazuia wasichana kuendelea na masomo kutokana na ndoa za kulazimishwa. | Jinsia | Sheria na Katiba, Jumuiya huru za kiraia, Maendeleo ya Jamii Jinsia na Watoto |
| | | • Fanya ardhi iweze kutumika kama dhamana ya kupata mikopo na kuboresha matumizi na usimamizi wa ardhi ikiwa ni pamoja na kupanda miti na kupunguza ufugaji wa mifugo mingi kupita kiasi (overstocking). | Fedha, ardhi, mazingira | Ardhi na maendeleo ya makazi, Fedha, Maliasili na utalii, Kilimo na uhakika wa chakula, sekta binafsi |
| | | • Ongeza kasi ya kuchukua hatua ya kutekeleza mikataba na kutatua migogoro ya kibiashara. | Sheria | Sheria na Katiba, Sekta binafsi |
| | | • Imarisha kanda za uzalishaji kwa ajili ya soko la nje; Imarisha taratibu za kuwapa dhamana ya mikopo wafanya biashara na wazalishaji wadogo na wa kati; Tekeleza kikamilifu Sera na mpango wa Kuwaendeleza wafanyabiashara wadogo na wa kati. Endeleza/anzisha utaratibu wa kuwasaidia wafanyabiashara wadogo na wa kati ili waweze kusimamia vyema biashara zao. | Biashara ndogo ndogo na za kati (SMEs) | Viwanda na Biashara, Sekta binafsi |
| | | • Saidia taasisi zinazowezesha maendeleo ya teknolojia na kupata teknolojia mpya na toa motisha kwa kuanzisha teknolojia rahisi na sahihi; na boresha uwezo wa sekta binafsi kutumia teknolojia hizo | Sayansi na teknolojia | Viwanda na biashara, Sayansi teknolojia na elimu ya juu, Elimu na Utamaduni, Fedha, Sekta binafsi Jumuiya huru za kiraia |

| Malengo | Matokeo ya kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| | biashara cha 14% ifikapo 2010.<br><br>Punguza kiwango cha ukosefu wa ajira kutoka 12.9% mwaka 2000/01 hadi (xxx) ifikapo 2010 na kushughulikia matatizo ya kutokutumia vyema fursa za ajira (underemployment) vijijini. (WKMVM)<br><br>Ongeza mchango wa sekta za viwanda katika Pato Ghafi la Taifa kutoka xxx hadi xxx mwaka 2010. (WVB)<br><br>Ongeza ubunifu wa teknolojia, endeleza, boresha na tumia teknolojia<br><br>Ongeza usawa wa mikoa katika ukuaji uchumi<br><br>Punguza athari za uzalishaji kwa mazingira na maisha ya watu.<br><br>Ingiza masuala ya jinsia katika uchumi mpana na katika sera na mikakati ya sekta.<br><br>Punguza uharibifu wa ardhi na upotevu wa Bioanuai | • Saidia taasisi zinazokuza uwekezaji, ajira na ukuaji wa kipato, mfano biashara ndogo na za kati katika sekta ya uzalishaji na huduma ikiwa ni pamoja na shughuli za usindikaji wa mazao ya kilimo na uzalishaji. | Ajira, sekta binafsi Wafanyabiashara wadogo na wa kati | Viwanda na Biashara, Kazi maendeleo ya vijana na michezo, SIDO, VETA, Sekta binafsi |
| | | • Ongeza uwekezaji wa umma/serikali ili kuwezesha upatikanaji wa ajira kwa lengo la kupunguza umasikini na endeleza/ongeza uwezekazaji wa sekta binafsi katika sekta zinazoongoza katika kuchangia ukuaji wa uchumi ikiwemo utalii, madini na viwanda. | Utalii na madini | Fedha, Nishati na madini, Viwanda na Biashara, Maliasili na Utalii, Mabenki, Sekta Binafsi, Jumuiya huru za kiraia |
| | | • Andaa na tekeleza hatua za kusaidia na kuongeza tija na usalama wa wachimbaji wadogo wadogo wa madini na kupunguza uharibifu wa mazingira. | Madini, Mazingira | Nishati na Madini, Jumuiya huru za kiraia, Sekta binafsi, Ofisi ya Makamu wa Rais, NEMC |
| | | • Anzisha na tekeleza mikakati ya mikoa na sekta kuhusu uwekezaji kwa lengo ya kuongeza ajira na kukuza uzalishaji | Sekta mbalimbali | Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo, Sekta binafsi, Jumuiya huru za kiraia |
| | | • Tekeleza Programu ya kuboresha mazingira ya biashara (BEST) na tekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Biashara. | Biashara, Wafanyabiashara wadogo na wa kati | Viwanda na Biashara, Fedha, Kituo cha uwekezaji, TRA, Sekta binafsi, Mipango Ubinafsishaji |
| | | • Imarisha vyombo vya kuweka na kutekeleza viwango vya kuhusu masuala ya kazi (labour) kwa ajili ili kuwezesha majadiliano na kuboreshwa kwa maslahi na masharti ya ajira, kuleta utulivu katika sehemu za kazi na kuongeza tija katika viwanda na biashara. | Kazi, Sheria, Sekta binafsi | Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo, Sheria na Katiba, Vyama vya waajiri, vyama vya wafanyakazi |
| | | • Himiza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kuwekeza katika mafunzo ya biashara, masoko ya nje na mafunzo katika kuhakikisha ubora na kuanzisha vituo vya kudhibiti ubora vilivyo na teknolojia/maabara za kisasa. Panua huduma za upimaji wa hali ya hewa, udhibiti wa viwango na utoaji wa hati za ubora. | Biashara, Uwekezaji, kujenga uwezo | Fedha, Kituo cha Uwekezaji, viwanda na biashara, Sekta binafsi, Shirika la Viwango (TBS) |
| | | • Panua na boresha mawasiliano ya reli, barabara kuu, bandari, viwanja vya ndege na huduma za usafiri/usafirishaji kwa kuimarisha ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi. | Usafirishaji na miundombinu | Ujenzi, Mawasiliano-Uchukuzi, Mipango Ubinafsishaji, Bandari, Sekta binafsi |
| | | • Panua mtandao wa mawasiliano (huduma za posta, ujuzi wa kutumia kompyuta, mawasiliano ya simu ikilinganishwa na idadi ya watu na mtandao wa internet). | Miundombinu | Ujenzi, TPC, Sekta binafsi, Elimu na Utamaduni, TTCL, TACRA |
| | | • Pitia sheria za uanzishaji wa taasisi za utafiti na maendeleo; na kuza matumizi ya kibiashara ya teknolojia zilizothibitika. | Teknolojia | Biashara na viwanda, TIRDO, CAMARTEC, TBS |
| | | • Andaa mpango wa utekelezaji na tekeleza sera ya ajira: Anzisha na endeleza kituo cha habari kuhusu soko la ajira. | Ajira | Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo, waajiri wote, Jumuiya huru za kiraia |
| | | • Imarisha taasisi na uwezo wa watendaji ili kuratibu vyema utoaji wa huduma za ajira nchi nzima | Ajira | Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo, TAMISEMI, Sekta binafsi, Taasisi za mafunzo |
| | | • Endelea na utekelezaji wa programu ya kuendeleza stadi zinazohitajika katika soko la ajira, kwa lengo la kuongeza ajira binafsi na kukuza tija. | Uwezo wa watu | Elimu na Utamaduni, Sekta binafsi, taasisi za elimu |
| | | • Chukua hatua mahsusi na za makusudi za kubuni fursa za ajira kwa makundi ya watu walio katika hatari zaidi ya kuangukia katika umasikini ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu. | Ajira, Ulemavu, Jinsia | Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo, Sekta binafsi, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Uwekezaji wa serikali katika miundombinu na kazi nyingine unaongeza moja kwa moja ajira kwa jamii au unaongeza fursa za ajira kwa kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi. | Miundombinu, Ajira | TAMISEMI na Ujenzi |
| | | • Panua mtandao wa barabara na kuzifanyia matengenezo ili kuziongezea hadhi na ubora wake, jenga na karabati barabara kuu za kitaifa, barabara za wilaya na barabara zinazounganisha vijiji – tengeneza fursa za ajira za moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa jamii na kuchochea ukuaji wa sekta binafsi. | Barabara | Ujenzi, TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi, jamii |


| Malengo | Matokeo ya kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| | | • Anzisha na tekeleza programu ya jamii ya ujenzi na matunzo ya barabara za vijijini na mijini inayotegemea nguvu kazi (labour intensive) na inayotekelezwa kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. | Ajira, Jinsia, barabara | Ujenzi, TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi, jamii |
| | | • Endeleza biashara na kuchagiza na kutetea kuwepo kwa biashara ya haki na utandawazi unaojawajumuisha watu wote na kujali maslahi yao. Jenga uwezo wa kutoa huduma za kibiashara ili kuweza kunufaika na uzalishaji unaolenga soko la kimataifa, kutumia utaalamu kutoka kwa watu wengine na mitandao ya masoko. Imarisha taratibu za udhamini wa wafanyabiashara wanaopeleka bidhaa katika masoko ya nje. | Biashara | Fedha, Viwanda na Biashara, Benki Kuu |
| | | • Jenga uwezo wa watu katika kufanya majadiliano ya kibiashara; oanisha viwango na boresha taratibu za forodha na fungua masoko kwa ajili ya biashara na fedha. Imarisha jitihada zinazoendelea hivi sasa za kuongeza ushiriki wa wanawake katika masoko ya kikanda na ya kimataifa. | Biashara, Wafanyabiashara wadogo na wa kati | Fedha, Viwanda na Biashara, Benki Kuu, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| | | • Boresha mazingira ya biashara (upatikanaji wa mikopo, taratibu za biashara, haki ya kumiliki mali, leseni za ukodishaji ardhi na kodi); ongeza kasi ya taratibu za usajili wa biashara kwa kuondoa taratibu zisizo za lazima. | Biashara | Fedha, TRA, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Viwanda na Biashara. |
| | | • Sekta zote kuendeleza na kuhimiza kujumuishwa kwa hatua au shughuli za uhifadhi wa mazingira katika mipango na mikakati yao; kuhakikisha utekelezaji wa hatua za usimamizi na tathmini ya athari za shughuli zao kwa mazingira. | Mazingira | Sekta za Uzalishaji na utoaji huduma, Ofisi ya Makamu wa Rais, NEMC, Jumuiya Huru za Kiraia, Kilimo na Uhakika wa Chakula na Viwanda na Biashara |
| | | • Andaa mpango wa utekelezaji ili kusimamia utekelezaji wa sheria ya usimamizi wa mazingira inayoandaliwa hivi sasa. | Mazingira | Ofisi ya Makamu wa Rais, Maliasili na Utalii, Kilimo na Uhakika wa Chakula na Madini na Nishati |
| | | • Endeleza matumizi ya teknolojia ya mawasiliano na matumizi ya mawasiliano ya kompyuta katika uendeshaji wa shughuli za serikali (e-government) | Teknolojia | Biashara na viwanda, Mawasiliano na Uchukuzi, Sayansi, teknolojia elimu ya juu, sekta binafsi |
| | | • Elekeza matumizi ya fedha za serikali katika malengo ya kipaumbele na shughuli zinazolenga kufikiwa kwa malengo hayo – msisitizo ukiwekwa katika shughuli za kuzuia kuenea kwa maambukizo ya VVU/UKIMWI na kuhakikisha kuwa rasilimali hizo zinakwenda moja kwa moja kwa mamlaka za serikali za mitaa zinazohusika (kushughulikia mahitaji ya wilaya zilizo nyuma kimaendeleo) | Serikali za mitaa | TAMISEMI, Fedha, ALAT, Jumuiya Huru za Kiraia |
| 3) Inua/boresha upatikanaji wa chakula, uwezo wa kukitumia chakula hicho na lishe katika ngazi ya kaya (msisitizo ukiwekwa katika mahitaji ya uhakika wa chakula ya | Ongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani milioni 9 mwaka 2003/04 hadi tani milioni 10 ifikapo 2010. (WKUC)<br>Punguza utapiamlo (kiwango cha uzito pungufu wa watoto) kutoka 29% mwaka 2000/01 hadi 20% mwaka 2010. (TFNC/WA)<br>Punguza kiwango cha watoto kudumaa (wasting) kutoka 5.4% mwaka 2000/01 hadi 2 | • Toa ruzuku kwa pembejeo kwa uzalishaji wa mazao ya chakula yaliyochaguliwa. | Kilimo | Kilimo na Uhakika wa Chakula, Fedha, Ushirika na Masoko |
| | | • Tafiti, bainisha na endeleza vifaa na teknolojia rahisi ya uhifadhi wa chakula katika maeneo ya vijijini | Kilimo, utafiti | Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Taasisi za utafiti, Jumuiya huru za kiraia. |
| | | Boresha mtandao wa barabara ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya chakula kutoka katika maeneo yenye ziada ya mazao hayo. | Barabara na masoko | Ujenzi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta binafsi |
| | | Kamilisha sera ya uhakika wa chakula na andaa mkakati na mpango wa utekelezaji wa uhakika wa chakula | Kilimo | Taasisi ya Chakula na Lishe, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sekta binafsi |

| Malengo | Matokeo ya kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| | mwaka 2010 (TFNC/WA)<br><br>Punguza matukio ya upungufu wa damu (WA) | Kusanya takwimu zilizochanganuliwa kijinsia kuhusu matokeo yanayofikiwa katika nyanja za afya, lishe na elimu, uwezo wa kupata na kutumia mali na miundombinu na kunufaika nayo, mazingira ya kazi na ajira, na ukatili wa kijinsia. | Ukusanyaji wa takwimu na ufuatiliaji | Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Sekta zote, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| 4) Umasikini wa kipato wa wanaume na wanawake wa vijijini umepungua kwa kiwango kikubwa. | Punguza kiwango cha umasikini wa watu (wanaume na wanawake) waishio vijijini wasioweza kukidhi mahitaji yao ya msingi (below basic need poverty line) kutoka 38.6% mwaka 2000/01 hadi kufikia 24% mwaka 2010.<br><br>Punguza kiwango cha watu waishio vijijini (wanaume na wanawake) walio masikini wa chakula kutoka 27% mwaka 2000/01 hadi 14% mwaka 2010.<br><br>Ongeza tija na uwezekano wa kupata faida katika shughuli za zilizo ndani na nje ya sekta ya kilimo.<br><br>Sera za kilimo kujumuisha haki za wanawake huku kukiwa na ongezeko la fursa za wanawake kupata na kutumia ardhi, mikopo na biashara.<br><br>Ongeza kiwango cha ukuaji wa kilimo kutoka 5% mwaka 2002/03 hadi 10% ifikapo mwaka 2010.<br><br>Ongeza kiwango cha ukuaji wa sekta ndogo ya ufugaji/mifugo kutoka 2.7% mwaka 2000/01 hadi 9% ifikapo mwaka 2010.<br><br>Ongeza kiwango cha ukuaji wa mazao ya biashara yanayouzwa nje ya nchi kutoka 6.8% mwaka 2002/03 hadi 9% ifikapo mwaka 2010. | Vutia uwekezaji wa umma na sekta binafsi katika sekta kuu za kilimo (ikiwa ni pamoja na mifugo) na maliasili; | Kilimo | Sekta binafsi, Wizara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula, Ushirika na Masoko, Maliasili na Utalii, Ardhi na Maendeleo ya Makazi |
| | | Kuza na endeleza ujuzi na mafunzo ya biashara kwa wananchi wa maeneo ya vijijini hususan wanawake na vijana | Kilimo, biashara, maendeleo ya watu, jinsia na vijana | Elimu na Utamaduni, Maendeleo ya jamii Jinsia na Watoto, Kazi maendeleo ya Vijana na Michezo, Ushirika na Masoko, VETA, SIDO, TAMISEMI, Jumuiya huru za kiraia. |
| | | Kuza na endeleza mipango ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, uvuvi, bidhaa za misitu, wanyama pori na bidhaa za mifugo n.k | Kilimo, misitu, wanyamapori, uvuvi, biashara | Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maliasili na Utalii, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Sekta binafsi, Jumuiya huru za kiraia, Viwanda na Biashara, SIDO |
| | | Ongeza fursa ya wananchi kutumia mitambo na teknolojia rahisi na sahihi katika uzalishaji wao | Sayansi na Teknolojia | Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, taasisi za utafiti, Sekta binafsi, Jumuiya huru za kiraia, CARMARTEC |
| | | Boresha/inua uwezo wa wakulima wadogo wadogo kupata pembejeo kwa kutoa ruzuku na kuongeza fursa ya kupata mikopo midogo midogo. | Kilimo na masoko | Sekta binafsi, Jumuiya huru za kiraia, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Masoko na Ushirika, Fedha. |
| | | Inua uwezo wa vijana na wanawake kupata na kutumia rasilimali za uzalishaji, mfano, ardhi na maliasili. | Vijana, Jinsia, ardhi | Ardhi na maendeleo ya Makazi, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maji na maendeleo ya mifugo, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya huru za kiraia, Maliasili na Utalii, Ofisi ya Makamu wa Rais |
| | | Boresha na ongeza huduma za ushauri hususan huduma za utafiti na ughani ili kukidhi mahitaji ya wakulima na wafugaji wadogo. | Kilimo, mifugo | Maji na maendeleo ya Mifugo, Kilimo na Uhakika wa Chakula, taasisi za utafiti, Jumuiya huru ya kiraia, Sekta Binafsi |
| | | Ongeza idadi ya miradi ya umwagiliaji na endeleza matumizi mazuri ya maji katika miradi yote. | Kilimo, maji | Maji na maendeleo ya Mifugo, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Sekta Binafsi, Taasisi za utafiti, |
| | | Tumia vyema na kwa ufanisi maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za ufugaji , jenga uwezo wa taasisi za wafugaji na ongeza tija katika ufugaji. | Ardhi, Ufugaji, Mazingira, Mifugo | Maji na maendeleo ya Mifugo, Jumuiya huru ya kiraia, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, TAMISEMI, Jamii. |
| | | Jenga maeneo zaidi ya kunyweshea mifugo maji; boresha ubora wa huduma za matibabu ya mifugo na upatikanaji wake na endeleza viwanda vya maziwa na ngozi (Wafanyabiashara wadogo na wa kati) | Maji, Mifugo, viwanda | Maji na maendeleo ya Mifugo, Viwanda na Biashara, TAMISEMI, Jamii, Sekta Binafsi |

| Malengo | Matokeo ya kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| | Badilisha sekta ya ukulima mdogo mdogo kuwa ya wazalishaji wadogo wa kibiashara.<br><br>Pata na wezesha upatikanaji wa masoko kwa bidhaa za kilimo.<br><br>Kuza na endeleza shughuli za kilimo.<br><br>Karabati kilomita 15,000 za barabara za vijijini ifikapo mwaka 2010 kutoka kilomita 4,500 mwaka 2003.<br><br>Ongeza mchango wa wanyamapori, misitu na uvuvi katika kipato cha jamii za vijijini | Inua tija katika shughuli za sasa za kilimo kwa kuwekeza na kuanza kutumia teknolojia za kisasa za uzalishaji katika kilimo (kilimo na mifugo). | Kilimo na mifugo | Maji na Maendeleo ya Mifugo, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Sekta binafsi, taasisi za utafiti, Jumuiya huru za kiraia, Wakulima |
| | | Anza kuzalisha mazao ya biashara yenye faida kubwa zaidi, na tafuta masoko na bidhaa mpya, ongeza gharama ya bidhaa zinazozalishwa na tumia fursa mpya za kupata malighafi nchini. | Kilimo na Masoko | Sekta binafsi, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Mawasiliano na Uchukuzi. |
| | | Boresha usafiri/usafirishaji, punguza gharama za usafirishaji na boresha utafutaji wa masoko ili kuwahakikishia wazalishaji faida kubwa zaidi. | Usafirishaji na Miundombinu | Ujenzi, TAMISEMI, Sekta binafsi, Jumuiya huru za kiraia |
| | | Wekeza katika miundombinu na ongeza uwezo wa wazalishaji kuyafikia masoko ya ndani ya nchi, ya kanda na ya kimataifa ili kuongeza tija na kipato katika kilimo. | Miundombinu | Ushirika na Masoko, Fedha, Ujenzi, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, |
| | | Kuza na endeleza ushiriki wa wananchi katika michakato ya kufanya maamuzi na kutayarisha mipango hasa katika ngazi za vijiji na wilaya kwa kuhakikisha kuwa wanawake na vijana wanawakilishwa kikamilifu. | Utawala | TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Jumuiya huru za kiraia, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ushirika na Masoko, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto |
| | | Weka miundo mbinu ya kutosha inayohitajika kukabiliana na mahitaji ya malengo ya kupunguza umasikini – Jenda uwezo wa kukarabati kilomita 15,000 za barabara za vijijini ifikapo mwaka 2010 kutoka kilomita 4,500 mwaka 2003. (WU & TAMISEMI) | Barabara | Ujenzi, TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa Sekta binafsi, Jumuiya huru za kiraia |
| | | Shirikisha jamii za vijijini katika kujenga na kusimamia barabara za vijijini. | Ajira, miundombinu | Ujenzi, TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa Sekta binafsi, Jumuiya huru za kiraia Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto |
| | | Ongeza upatikana wa huduma za fedha kwa wakulima wadogo wadogo na ukilenga zaidi kwa vijana na wanawake na endeleza shughuli za uzalishaji vijijini zisizo za kilimo, msisitizo ukiwekwa katika kuanzisha viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo (agro processing industries). | Mikopo, vijana, jinsia | Kilimo na Uhakika wa Chakula, Ushirika na Masoko, Mabenki, Jumuiya huru za kiraia, TAMISEMI, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto |
| | | Anzisha programu za kuendeleza na kuongeza fursa za watu wa vijijini wanawake na wanaume kushiriki katika shughuli za kuzalisha kipato kwa kuendeleza viwanda vidogo vidogo, uzalishaji wa mazao yasiyo asilia, sanaa za mikono za kiasili, mradi midogo ya umwagiliaji maji kwa kutumia uvunaji wa maji ya mvua. | Ajira, Jinsia | Sekta za uzalishaji, TAMISEMI, Sekta Binafsi, Jumuiya huru za kiraia |
| | | Kuza na endeleza vyama/miradi ya jamii ya kuweka na kukopa kama vile SACCOS na mifuko ya kuweka na kukopa. | Fedha na mikopo, jinsia | Kilimo na Uhakika wa Chakula, Ushirika na Masoko, Mabenki, Jumuiya huru za kiraia, TAMISEMI, Biashara ndogo na za kati, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na watoto |
| | | Chukua hatua za kuhakikisha uthabiti wa bei (price stabilisation) mathalan kwa kuweka vyombo vya udhibiti ili kuzuia kuwa na magenge (cartels) ya wafanyabiashara kwa ajili ya kuweka njama ya kupanga bei ya pamoja isivyo halali. | Fedha | Fedha, Viwanda na Biashara, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ushirika na Masoko |
| | | Toa nishati ya kuaminika na ya gharama nafuu kwa maendeleo ya uchumi. | Nishati, teknolojia | Nishati na Madini, Mamlaka za Serikali za Mitaa, sekta binafsi, TANESCO |
| | | Weka msisitizo wa kipekee katika kufikisha huduma ya umeme vijijini kwa lengo la kuwapunguzia wanawake mzigo wa kazi. | Nishati, jinsia | Nishati na Madini, TANESCO sekta binafsi |
| | | Wezesha upatikanaji wa nishati mbadala kwa maeneo ya vijijini na miradi ya matumizi mazuri ya nishati inayosaidia kupunguza matumizi ya nishati na kuwapunguzia wanawake mzigo wa kazi. | Nishati, jinsia | Nishati na Madini, Taasisi za Utafiti, Jumuiya huru za kiraia, sekta binafsi |

| Malengo | Matokeo ya kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| | | Boresha na ongeza upatikanaji wa huduma ya kuaminika ya maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mahitaji ya uzalishaji kwa lengo la kuwapunguzia mzigo wa kazi wanawake, wasichana na watoto. | Maji, mazingira, jinsia | Maji na Maendeleo ya Mifugo, Maliasili na Utalii, Mamlaka za serikali za Mitaa, jumuiya huru za kiraia |
| | | Hakikisha usimamizi endelevu wa maeneo ya vyanzo vya maji na utunzaji wa misitu katika maeneo muhimu ya nyanda za juu yenye vyanzo vya maji. | Misitu, maji, nishati, mazingira | maliasili na utalii, mamlaka za serikali za mitaa, jumuiya huru za kiraia, ofisi ya makamu wa rais, NEMC |
| | | Panua shughuli za maendeleo ya jamii, mfano, shughuli za jamii za ujenzi wa barabara zinatotegemea nguvu kazi - na kuimarisha programu kama za SIDO (Viwanda vidogo vidogo) TASAF na SELF nk, ambazo zinalenga katika ngazi ya jamii (micro-level). | Maendeleo ya jamii, ajira, jinsia | Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kazi Maendeleo ya Vijana na Michezo, Elimu na Utamaduni, Sheria na Katiba, Jumuiya Huru za Kiraia, Jamii |
| | | Ainisha na pitia sheria, na endesha kampeni za utetezi dhidi ya mila na tamaduni zinazowanyima wanawake na vijana fursa ya kupata rasilimali za uzalishaji na fedha (Viwanda na Biasharaaji) - ikiwa ni pamoja na sheria ya mirathi na haki yao ya kumiliki mali binafsi. | Sheria, jinsia, vijana | sheria na katiba, ardhi na maendeleo ya makazi, maendeleo ya jamii, jinsia na watoto, jumuiya huru za kiraia |
| | | Elimisha jamii kuhusu haki za msingi za mtoto ikiwa ni pamoja na kupiga vita ajira ya watoto. | Watoto | maendeleo ya jamii, jinsia na watoto, elimu na utamaduni, mamlaka za serikali za mitaa, kazi maendeleo ya vijana na michezo, jumuiya huru za kiraia |
| | | Anzisha na chochea utalii wa ndani na shughuli za biashara ndogo ndogo zinazoendana na sekta ya utalii | Utalii, jinsia | maliasili na utalii, sekta binafsi, jumuiya huru za kiraia, Biashara ndogo na za kati |
| | | Anzisha programu za kuongeza udhibiti na mapato ya jamii katika maeneo ya usimamizi wa wanyamapori na anzisha mifuko ya usimamizi wa maliasili inayosimamiwa na jamii zenyewe, tumia ujuzi wa asili wa eneo husika. | Wanyamapori, utalii, ajira, jinsia | MALIASILI NA UTALII, MAMLAKA ZA SERIKALI ZA Mitaa, Sekta binafsi, Jumuiya huru za kiraia |
| | | Inua/kuza mwamko na ufahamu wa wananchi kuhusu VVU/UKIMWI kwa lengo la kubadilisha tabia katika maeneo ya uzalishaji vijijini ikiwa ni pamoja na maeneo yenye migodi. | VVU/UKIMWI | TACAIDS, sekta zote, sekta binafsi, jumuiya huru za kiraia |
| | | Anzisha programu za VVU/UKIMWI mahali pa kazi katika sekta zote na sekta binafsi *(Zingatia: Mkakati huu unaohusiana na mikakati katika eneo 2 kuhusu VVU/UKIMWI)* | VVU/UKIMWI | Sekta na Waajiri wote, TACAIDS, Jumuiya huru za kiraia |
| | | Sera na mikakati katika sekta zinazohusu maliasili zimeoanishwa na kuondoa migongano yote katika sheria na taratibu. Boresha hatua za uhifadhi wa ardhi na endeleza mipango ya jamii kusimamia maliasili. | Sheria,maliasili, utawala | Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais Ikulu, Jumuiya huru za kiraia |
| | | Tekeleza mipango ya matumizi na usimamizi mzuri wa ardhi – makazi yaliyopangwa/yaliyopimwa – Sheria ya Ardhi ya 1999, na boresha makusanyo ya mapato yatokanayo na ardhi na mifumo ya usimamizi wa fedha. | Ardhi, makazi | Ardhi na Maendeleo ya Makazi, TRA, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Jumuiya huru za kiraia, Fedha |
| 5) Umasikini wa kipato wa wanaume na wanawake wa mijini umepungua | Punguza kiwango cha watu (wanaume na wanawake) waishio mijini wasioweza kukidhi mahitaji yao ya msingi kutoka 25.8% mwaka | Saidia Wafanyabiashara wadogo na wa kati (hasa katika uzalishaji unaohusu kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mathalan usindikikaji mazao) na sekta isiyo rasmi kwa kutoa mikopo, kuboresha mazingira ya biashara na msaada wa teknolojia. Wezesha uwekezaji binafsi na wa umma kwa lengo la kukuza ajira. | Biashara ndogo na za kati (SMEs), Sekta isiyo rasmi, teknolojia | Viwanda na Biashara, Fedha, Mabenki, Taasisi za utafiti, Jumuiya huru za kiraia, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Elimu na Utamaduni, SIDO |

| Malengo | Matokeo ya kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika |
|---|---|---|---|---|
| | 2000/01 hadi kufikia 12.9% mwaka 2010 (OMR).<br><br>Punguza kiwango cha watu waishio mijini (wanaume na wanawake) walio na umasikini wa chakula kutoka13.2% mwaka 2000/01 hadi 6.6% mwaka 2010.<br><br>Kuza na endeleza ajira binafsi na ongeza fursa za ajira katika sekta isiyo rasmi.<br><br>Ongeza kiwango cha vijana na wanawake walio katika sekta rasmi na biashara. (WKMVM)<br><br>Saidia Wafanyabiashara wadogo na wa kati (SMEs) na sekta isiyo rasmi<br><br>Punguza kiwango cha watoto walio katika ajira nchi nzima kutoka 25% hadi pungufu ya 10% ifikapo mwaka 2010 na wawezeshe kushiriki katika shughuli mbadala ikiwa ni pamoja na kuwaandikisha katika shule za msingi, MEMKWA na mafunzo ya ufundi stadi | Kuza na endeleza ubora wa nguvu kazi kwa kuwa na programu za mafunzo kwa vitendo (apprenticeship) na ujasiriamali/biashara (entrepreneurship) zinazowalenga vijana (ili waweze kukuza biashara zao); saidia programu za kuwaendeleza wafanya biashara wanawake na kutoa mafunzo kwa wasichana yatakayowawezesha kupata ajira. | Ajira, vijana, jinsia | Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, viwanda na Biashara, Elimu na Utamaduni, Jumuiya huru za kiraia, Sekta binafsi, SIDO |
| | | Tekeleza sera na sheria zinazoongeza fursa ya ajira kwa vijana na wanawake katika sekta isiyo rasmi, biashara na sekta rasmi, ili wawe na fursa sawa ya ajira na kutendewa sawa na wengine na kupata fursa sawa ya kumiliki mali binafsi. | Ajira, vijana, jinsia | Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Sheria na Katiba, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, TAMISEMI, Jumuiya huru za kiraia, Sekta binafsi, SIDO |
| | | Fufua vituo/vyuo vya mafunzo ya ufundi vinavyotoa mafunzo kwa watu wenye ulemavu na chukua hatua mahsusi na za makusudi (affimative action) za kongeza fursa za ajira kwa watu wenye ulemavu. | Ulemavu, ajira | Elimu na Utamaduni, Jumuiya huru za kiraia, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, VETA |
| | | Hakikisha upatikanaji wa uhakika na wa kuaminika wa huduma muhimu za kijamii ikiwemo nishati, maji safi na uondoaji wa maji taka katika maeneo ya mijini. | Nishati, maji, afya | Nishati na Madini, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Jumuiya huru za kiraia, Sekta binafsi |
| | | Kuwa na matumizi endelevu ya maliasili ili kuhakikisha kuwa nishati inaendelea kupatikana (ikiwa ni pamoja na misitu, vyanzo vya maji na uchomaji mkaa). | Nishati, misitu, mazingira | Maliasili na Utalii, TANESCO, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Jumuiya huru za kiraia |
| | | Tekeleza mpango kamambe wa nishati vijijini msisitizo ukiwekwa katika kuendeleza miradi ya kupeleka umeme vijijini, maendeleo ya vyanzo vingine endelevu vya nishati na kuunganisha maeneo yote katika gridi ya taifa. | Nishati, teknolojia, ajira | Nishati na Madini, TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, TANESCO, Taasisi za utafiti, Maliasili na Utalii, Fedha |
| | | Anzisha na tekeleza programu za kupunguza ajira mbaya ya watoto katika kila sekta. | Sekta mbalimbali | Vyama vya wafanyakazi, Vyuo vya mafunzo ya ufundi |
| | | *Angalia pia mikakati katika eneo 2 kuhusu malengo yanayohusu maji na usafi wa mazingira, maji taka, nk (sanitation).* | | |


MWAKA HUU WATOTO 500,000 WAMEMALIZA SHULE...
WAZIRI ELIMU
MWAKA HUU TUNA NAFASI ZA KAZI MPYA 20
WAZIRI KAZI
Nathan 2004
Seri K. anasema...
HAYA YAMEPITWA NA WAKATI... SASA TUTAZINGATIA STADI, UJUZI NA AJIRA

## Eneo la 2: Kuinua Ubora wa Maisha na Ustawi wa Jamii



# Eneo la 2: Kuinua Ubora wa Maisha na Ustawi wa Jamii

**Matokeo Makuu Tarajiwa:**

1. Kukua na kuimarika kwa ubora wa maisha na ustawi wa jamii, msisitizo wa kipekee ukielekezwa wa watu masikini zaidi na makundi yaliyo katika hatari kubwa zaidi ya kuwa masikini.
2. Kupungua kwa hali ya kutokuwepo usawa katika matokeo ya jitihada za kupunguza umasikini (mfano, katika elimu, uhai, afya) baina ya maeneo ya kijiografia, watu wa vipato, umri, jinsia na makundi tofauti.

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au Maeneo ya Ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| 1. Kuboreshwa na kuongezeka kwa fursa ya kupata elimu (access), umuhimu wa elimu itolewayo (relevance), na kiwango cha kufaulu wanafunzi (performance) katika ngazi za shule za msingi na sekondari, na watu wazima wote kujua kusoma na kuandika. | Ongeza kiwango na idadi ya uandikishaji wa wavulana na wasichana katika shule za msingi kutoka 90.5% mwaka 2004 hadi kufikia 99% mwaka 2009 (WEU)<br><br>Kupungua kwa idadi ya vijana walio katika mpango wa MEMKWA kutoka 234,000 mwaka 2004/05 hadi 70,566 mwaka 2007/08 (WEU).<br><br>Punguza idadi ya watu wazima wasiojua kusoma na kuandika kutoka milioni 3.8 mwaka 2004/5 hadi milioni 1.5 mwaka 2007/08.<br><br>Ongeza kiwango cha watoto wenye ulemavu wanaoandikishwa, wanaohudhuria na kumaliza shule kutoka 0.1% mwaka 2000 hadi 20% mwaka 2010 (WKMVM).<br><br>Ongeza kiwango cha watoto yatima na wale walio katika mazingira magumu wanaoandikishwa, wanaohudhuria na kumaliza shule kutoka 2% mwaka 2000 hadi 30% mwaka 2010 (WKMVM).<br><br>Ongeza asilimia ya wasichana na wavulana wenye ulemavu na OVCs wanaofaulu kwenda sekondari, wanaoandikishwa, wanaohudhuria na kuhitimu elimu ya sekondari ifikapo mwaka 2010 (WKMVM)<br><br>Angalau 50% ya wavulana na wasichana walio katika umri wa miaka 14-17 wanaandikishwa katika shule za sekondari (ngazi ya chini- kidato I-IV).<br><br>Angalau 25% ya wavulana na wasichana wanaandikishwa katika shule za sekondari (ngazi ya juu- kidato V- VI). | Hakikisha kuwa watoto wote ikiwa ni pamoja na wale wenye ulemavu, wasichana wanaopata ujauzito na watoto wengine wote walio katika makundi yanayonyimwa haki na yaliyo katika hatari ya kuwa masikini, wanapata fursa ya kupata na kumaliza elimu bora ya msingi. | Elimu, jinsia, watoto | Maji na Maendeleo ya Mifugo, Afya, Ujenzi, Tamisemi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Ushirika na Masoko, Sekta Binafsi, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | Wizara ya Elimu na Utamaduni kutekeleza mikakati ya kujumuisha katika programu zake za shule za msingi na sekondari mahitaji ya makundi maalumu yaliyo katika hatari zaidi ya kuangukia katika umasikini. | Elimu, makundi yaliyo katika hatari ya kuangukia kwenye umasikini | TAMISEMI, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | Hakikisha kuwa kuna shule maalumu zenye vifaa na zana zote zinazohitajika (zinazoweza kupatikana kwa gharama nafuu) katika kutoa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu na ambao hawawezi kushiriki katika shule za kawaida, hii ni kwa wale pia ambao wapo kwenye MEMKWA na MUKEJA kwa vijana na watu wazima. | Elimu, makundi yaliyo katika hatari ya kuangukia kwenye umasikini | Elimu na Utamaduni, Jamii |
| | | Boresha na ongeza fursa ya watoto wote kupata elimu bora ya sekondari ambayo haitawabagua masikini, walemavu na makundi mengine ya watoto walio katika mazingira magumu. | Elimu, makundi yaliyo katika hatari ya kuangukia kwenye umasikini | Elimu na Utamaduni |
| | | Weka kipaumbele katika maendeleo, utoaji fedha na utekelezaji wa programu za nchi zinazosaidia kuendeleza elimu ya watoto yatima na wale walio katika mazingira magumu. | Elimu, makundi yaliyo katika hatari ya kuangukia kwenye umasikini, ustawi wa jamii. | Elimu na Utamaduni, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| | | Ongeza kiwango cha wanafunzi kuendelea kubaki shuleni na kumaliza elimu ya sekondari | Elimu, makundi yaliyo katika hatari ya kuangukia kwenye umasikini | Elimu na Utamaduni |
| | | Anzisha na weka taratibu rasmi za kutoa mafumzo kwa njia ya posta (distance learning) kwa vijana waliokosa nafasi ya kujiunga na elimu rasmi ya sekondari. | Elimu, makundi yaliyo katika hatari ya kuangukia kwenye umasikini | Elimu na Utamaduni |
| | | Tekeleza mipango na hatua maalumu za kuongeza fursa za wasichana kujiunga na kumaliza shule za sekondari; na kuinua kiwango chao cha kufaulu katika shule za msingi na sekondari. | Elimu | Elimu na Utamaduni |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au Maeneo ya Ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | Mazingira ya kujifunzia ya watoto wote shuleni yameboreshwa. (WEU)<br><br>Mahudhurio ya wanafunzi katika shule za msingi yanafikiwa kwa kiwango cha wastani wa angalau 85%. (WEU)<br><br>Angalau 95% ya wanafunzi walioanza pamoja shule pamoja wanamaliza darasa la 4.<br><br>Angalau 90% ya wanafunzi walioanza pamoja shule pamoja wanamaliza darasa la 7.<br><br>Angalau 60% ya wasichana na wavulana wanafaulu mitihani yao ya darasa la 7.<br><br>Angalau 70% ya wasichana na wavulana wanafaulu kwa kiwango cha daraja la I-III katika mitihani ya kidato cha nne<br><br>Mafunzo kuhusu VVU/UKIMWI na stadi za maisha yanatolewa katika shule zote za msingi na sekondari na vyuo vya ualimu.<br><br>Uwezo wa kujiunga, na ubora wa elimu katika shule binafsi umedhibitiwa (regulated).<br><br>Angalau 80% ya watu wazima, hususan wanawake katika maeneo ya vijijini wanajua kusoma na kuandika. | Endeleza sera ya sasa ya kutoa elimu ya msingi bure na kupunguza ada ya shule za sekondari ili kutoa fursa ya watoto wote kupata elimu. | Elimu | Elimu na Utamaduni, Sekta Binafsi |
| | | Weka malengo na viashiria sahihi vya kufikiwa mwaka 2010 vitakavyoashiria ubora wa jumla wa elimu ya sekondari (kidato cha I-IV na kidato cha V-VI). | Elimu | Elimu na Utamaduni |
| | | Hakikisha kuwa kuna usawa katika kuwapangia vituo vya kazi walimu wenye sifa na hamasa ya kazi na kuwapatia msaada wa kutoka (nyumba na mahitaji mengine muhimu), hususan, kwa walimu walio katika maeneo ya vijijini yasiyoweza kufikika kwa urahisi na wale wanaofundisha watoto wenye ulemavu. | Elimu | Jamii, Elimu na Utamaduni |
| | | Panua mafunzo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari ili kwenda sambamba na ongezeko la wanafunzi wanaoandikishwa. | Elimu | Sayansi, Elimu ya Juu, Elimu na Utamaduni |
| | | Fanya mageuzi katika mitaala ya shule za msingi na sekondari, mafunzo ya walimu, vifaa vya kufundishia, upimaji wa wanafunzi na mitihani na ukaguzi wa shule ili kukuza na kuendeleza ufundishaji na mazingira ya kujifunza yatakayowawezesha wanafunzi kuwa wadadisi, wabunifu na wenye stadi zinazotakiwa. Pitia upya mitaala ya mafunzo kwa walimu ili kujumuisha ufundishaji wa masuala yanayohusu VVU/UKIMWI | Elimu | Elimu na Utamaduni |
| | | Hakikisha kuwa uwiano wa kitabu kimoja cha kiada kwa mwanafunzi mmoja (1:1) unafikiwa katika shule za msingi na sekondari. | Elimu | Elimu na Utamaduni |
| | | Hakikisha kuwa walimu wa kutosha wa elimu maalumu wanapatiwa mafunzo na wale waliopo sasa wanapatiwa mafunzo kazini ili waweze kutoa elimu bora kwa watoto wenye ulemavu. Hakikisha kuwa watoto wanachunguzwa ili kubaini ulemavu na matatizo yao ya kiafya; hakikisha kuwa kuna vifaa maalumu vya kufundishia na kujifunzia vya kutosha kwa ajili ya watoto wenye ulemavu, hivyo ni pamoja na vifaa vya kuwawezesha kusikia, kanda zilizorekodiwa masomo yaliyo katika vitabu (audio-books), vitabu kwa ajili ya wasioona. Vifaa hivyo visambazwe mashuleni. | Elimu, Watoto, Ulemavu | Elimu na Utamaduni |
| | | Hakikisha kuwa ruzuku ya kila mtoto (capitation) na ya maendeleo kwa ajili ya shule za msingi na sekondari zinatolewa kwa ukamilifu wake, zinasambazwa katika ngazi ya shule kwa wakati na kuwa wazi kwa wote. | Elimu | Elimu na Utamaduni |
| | | Boresha uwezo na usawa wa kamati za shule kushiriki katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia ubora katika utoaji wa elimu katika ngazi za shule, ikiwa ni pamoja na uwazi katika matumizi ya fedha za shule. | Utawala | Elimu na Utamaduni |
| | | Panua na imarisha uwezo wa wakaguzi wa shule wa kufuatilia kikamilifu ubora wa elimu; hakikisha kuwa shule zote zinatoa elimu shirikishi na inayowawezesha wanafunzi kujifunza kwa dhati (active learning). | Elimu | Elimu na Utamaduni |
| | | Imarisha utekelezaji wa programu ya afya mashuleni | Elimu/Afya | Elimu na Utamaduni, Afya |
| | | uhakikisha kuwa shule zote za msingi na sekondari na programu za vijana walio nje ya shule zinatoa elimu bora ya kujikinga dhidi ya VVU/UKIMWI na stadi za maisha, kuanzia darasa la 3 au 4. | VVU/UKIMWI | TACAIDS, Elimu na Utamaduni, Jumuiya Huru za Kiraia/ Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au Maeneo ya Ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | | Boresha na jenga mahusiano mazuri ya kijinsia darasani na katika mazingira ya shule; toa mafunzo kwa walimu kuhusu mbinu shirikishi za kufundishia (interactive teaching methods), ajiri walimu wanawake waliopata mafunzo na wenye ari ya kazi, na tumia adhabu mbadala na zinazokubalika badala ya adhabu ya viboko. | Jinsia | Elimu na Utamaduni |
| | | Weka kipaumbele katika kutayarisha, kutenga fungu na kutekeleza programu endelevu za gharama nafuu za elimu ya watu wazima; Panua mafunzo kwa vitendo ya gharama nafuu yatakayowawezesha watu kujipatia ujira na kuendesha maisha yao. | Elimu | Elimu na Utamaduni |
| 2. Kupungua kwa vifo vya watoto, vifo na ulemavu kwa wanawake wajawazito na utapiamlo. | Punguza vifo vya watoto wachanga kutoka 90 hadi kufikia vifo 50 kwa kila watoto 1,000 wanaozaliwa hai.<br><br>Ongeza asilimia ya watoto walio chini ya miaka 2 waliopatiwa chanjo zote dhidi ya surua na DPT kutoka 80% mwaka 2002 hadi 85 mwaka 2010 (WA)<br><br>Ongeza matumizi ya vyandarua vilivyotiwa dawa ya kuua na kuzuia mbu (ITNs) kwa wanawake wajawazito na watoto. (WA/Malaria)<br><br>Punguza vifo vinavyotokea hospitalini vinavyosababishwa na malaria miongoni mwa watoto walio chini ya miaka 5 kutoka 12% mwaka 2002 hadi 8% mwaka 2010 (WA)<br><br>Punguza vifo vya watoto (walio chini ya miaka 5) kutoka 154 hadi kufikia vifo 79 kwa watoto 1,000 wanaozaliwa hai.<br><br>Punguza vifo vya akinamama wajawazito kutokana na matatizo ya uzazi kutoka vifo 529 hadi vifo 265 kwa wanawake 100,000 mwaka 2010.<br><br>Punguza kiwango cha watoto walio chini ya umiri mitano walio na kimo pungufu kuliko umri wao (stunting) kutoka 43.8% hadi kufikia 20% mwaka 2010 (WA) (TFNC)<br><br>Ongeza idadi ya watoto wanaozaliwa kwa kusaidiwa na wakunga wataalamu kutoka asilimia 50% hadi 80% ifikapo mwaka 2110 (WA) | Weka msisitizo katika mikakati ya afya ya umma na kinga ya maradhi kama vile kuhimiza matumizi ya vyandarua vilivyotiwa dawa (Viuatilifu), matumizi ya maji safi na salama, hatua za usafi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kushughulikiwa kwa maji taka na matumizi ya vyoo, kutoa elimu ya lishe na kutoa viini lishe (ili kutatua tatizo la upungufu wa viini lishe hivyo) kwa wanawake wajawazito na watoto wenye utapiamlo. | Afya, Elimu, maji, watoto, jinsia | Afya, TACAIDS, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Jumuiya Huru za Kiraia, Sekta Binafsi. |
| | | Endeleza na kuhimiza taratibu nzuri za kuwalisha na kuwanyonyesha watoto wachanga, msisitizo ukiwekwa katika haja ya wazazi kutoa matunzo yanayotakiwa kwa watoto na kuwalisha mara kwa mara. | Watoto, Afya | Afya |
| | | Ongeza ufahamu na mwamko wa wananchi kuhusu hatua rahisi na za gharama nafuu za kuzuia magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya maji. | Mazingira, Maji | Afya, Maji na Maendeleo ya Mifugo, |
| | | Tekeleza na panua mipango ya utoaji huduma muhimu za afya (essential health package) ya gharama nafuu, inayowafikia watu kwa urahisi na kwa ubora wa hali ya juu ili kushughulikia sababu kuu za vifo na ulemavu (ikiwa ni pamoja Mkakati wa kutibu Magonjwa ya Watoto kwa Uwiano (Intergrated Management of Childhood Illnesses - IMCI), lishe, afya ya uzazi na huduma ya dharura ya uzazi (emergency obstetric care), VVU/UKIMWI, malaria, magonjwa ya kuharisha kifua kikuu n.k). | Afya, VVU/UKIMWI | Afya |
| | | Tafiti uwezekano wa kuwa na mbinu madhubuti zaidi za kudhibiti malaria: matibabu ya haraka hasa kwa watoto walio chini ya miaka mitano na akina mama wajawazito; inua upatikanaji na hamasisha matumizi ya vyandarua vilivyotiwa dawa ya kuua na kufukuza mbu (viuatilifu); kuwa na mikakati ya kuongeza kiwango cha muda wa kuweka tena dawa katika chandarua chake (re-treatment rates) ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa dawa zinazodumu kwa muda mrefu zaidi; kupanua programu za udhibiti wa malaria (zinazofanyika hivi sasa kwa majaribio) kwa kuboresha mazingira (na kupanua ajira kwa vijana). | Afya, Jinsia, watoto | Afya, Tume ya Mazingira, Sekta Binafsi |
| | | Ongeza upatikanaji na ubora wa huduma za afya ya uzazi ikiwa ni pamoja na huduma za uzazi wa mpango, afya ya uzazi kwa vijana, huduma kwa mama wajawazito (antenatal care), huduma za dharura za uzazi (emergency obstetric care), huduma kwa mama baada ya kujifungua (post-natal care) na huduma kwa watoto wachanga. | Afya, Jinsia | Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| | | Ongeza rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya programu za kuzuia maambukizo ya VVU/UKIMWI ikiwa ni pamoja na programu za elimu kwa makundi mbalimbali ya jamii, kupanua huduma za upimaji na matibabu ya magonjwa ya ngono (STIs), huduma za ushauri nasaha upimaji wa hiari wa VVU, matumizi ya kondom n.k. | VVU/UKIMWI | Afya, Fedha, Sekta Binafsi, Jumuiya huru za Kiraia |


| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au Maeneo ya Ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | Punguza maambukizo ya VVU miongoni mwa wanawake wajawazito wenye umri wa kati ya miaka 15-24 kutoka 11% mwaka 2004 hadi 5% mwaka 2010 (WA)<br><br>Punguza maambukizo ya VVU miongoni mwa vijana wenye umri wa kati ya miaka 15-24 kutoka 11% mwaka 2004 hadi 10% mwaka 2010 (WA)<br><br>Punguza maambukizo ya VVU/UKIMWI miongoni mwa wanawake na wanaume wenye ulemavu (kuanzia umri wa miaka 15-35). (WKMVM)<br><br>Endeleza utoaji huduma wa kitaalamu (knowledge based care) miongoni mwa watoa huduma za afya ili pamoja na mambo mengine waweze kutoa huduma bora kwa walemavu na wazee.<br><br>Bodi na Kamati za Afya za kuendesha hospitali, vituo vya afya na zahanati zimeanzishwa na zinafanya kazi kikamilifu katika wilaya zote.<br><br>Makubaliano ya utoaji wa huduma (Service Agreement) yanatekelezwa na kuleta ufanisi.<br><br>Timu za Usimamizi wa Afya katika ngazi ya Mkoa (Regional Health Management Teams) zimeundwa na zinafanya kazi zake kikamilifu. | Ongeza na boresha huduma za matibabu kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, mbali na kutoa dawa za kurefusha maisha (AVR) kwa mfano, matibabu na kinga dhidi ya Kifua Kikuu na matibabu ya magonjwa mengine nyemelezi. | VVU/Kifua Kikuu | Afya, |
| | | Ongeza upatikanaji wa dawa za kurefusha maisha (ARVs) kwa haki/usawa, uendelevu na gharama nafuu, huku msisitizo ukiwekwa katika kutoa elimu kuhusu ARVs na kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. | VVU/UKIMWI | Afya, TACAIDS |
| | | Tekeleza programu ya kuendelea kuwahudumia watu wanaoishi na VVU/UKIMWI ikiwa ni pamoja na jitihada za kijamii kama vile, huduma za wagonjwa majumbani, msaada wa huduma muhimu mathalan, chakula na makazi mipira ya kuvaa mikononi (gloves) na msaada wa kisaikolojia. Endeleza na tekeleza programu zinazolenga kuwasaidia wajane wazee wanaotoa matunzo kwa watoto yatima na watu wanaoishi na VVU/UKIMWI. | VVU/UKIMWI, Jinsia | Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia, Vikundi vya Kijamii. |
| | | Unganisha jitihada za jamii za kuwahudumia watu wenye maradhi makubwa na ya muda mrefu kama vile VVU/UKIMWI, Kifua Kikuu na magonjwa ya moyo na hospitali au vituo vya afya vinavyotoa huduma maalumu kwa magojwa hayo, chini ya mpango wa kuendeleza matunzo na matibabu kwa wagonjwa hao. | VVU/UKIMWI, Jinsia | Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, TACAIDS, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | Jumuisha katika shughuli za kawaida za kila siku, hatua za kutatua tatizo la kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia ambalo linasababisha kiwango kikubwa cha maambukizi ya VVU/UKIMWI miongoni mwa wanawake na wasichana. | Jinsia | Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, TACAIDS, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | Ajiri na sambaza kwa usawa wahudumu wa afya, msisitizo ukielekezwa katika maeneo yenye upungufu wa wahudumu hao, hii ni pamoja na kuondoa vikwazo vya sasa katika kuajiri na kuwasambaza wafanyakazi katika maeneo mbalimbali, kuziwezesha halmashauri kuajiri, kuweka utaratibu wa kutoa motisha kwa "kada/nafasi zenye kazi ngumu"na kurekebisha taratibu za uhamisho ili ziwe rahisi zaidi. | Afya | Afya, TAMISEMI |
| | | Tathmini na hakiki kwa undani mkakati wa kuendeleza rasilimali ya watu katika sekta ya afya ili kuainisha upungufu wa taaluma mbalimbali miongoni mwa wafanyakazi wa sekta hiyo na kutekeleza mpango wa kutoa mafunzo haraka katika maeneo muhimu. | Elimu ya afya | Afya, |
| | | Kuhakikisha kuwa watoa huduma za afya katika ngazi zote wanakuwa na fursa sawa ya kupata kwa wakati taarifa zote muhimu kuhusu huduma za afya wanazoweza kuzitumia. | Afya | Afya, |
| 3. Punguza hatari itokanayo na uchafuzi wa mazingira na boresha afya/usafi wa mazingira na makazi. | Ongeza kiwango cha wakazi wa vijijini wanaopata maji safi na salama kutoka 53% mwaka 2003 hadi 65% mwaka 2009/10. Na kutoka 73% hadi 90% kwa wakazi wa mijini katika kipindi hicho.<br>(WMMM) | Kamilisha uanzishaji wa Bodi na Kamati za Afya na hakikisha kuwa katika bodi na kamati hizo kuna uwakilishi mpana ikiwemo wa makundi yanayowekwa pembezoni na kunyimwa haki za kimsingi. Hakikisha kuwa kamati hizi zinafanya kazi zake za kuhakikisha ubora katika utoaji wa huduma za afya na upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi. | Afya | Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| | | Timu za Usimamizi wa Afya katika ngazi ya Mkoa zimeundwa na zina uwezo wa kutoa msaada wa kutosha na wenye mwafaka kwa Timu za Usimamizi wa Afya katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya, huku zikiwa na majukumu na mamlaka yaliyoainishwa wazi na kwa ufasaha. | Afya | Afya |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au Maeneo ya Ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | Ongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma zilizoboreshwa za maji taka na vyoo kutoka 17% mwaka 2003 hadi 30% mwaka 2010 katika maeneo ya mijini (WMMM)<br><br>Punguza kiwango cha uchafuzi wa mazingira unaosababisha uchafuzi wa maji kutoka 20% mwaka 2003 hadi 10% mwaka 2010 (WMMM)<br><br>Ongeza idadi ya watu wenye kumiliki mali/ardhi wanawazoweza kutumia kama dhamana ya kupatia mikopo na hakikisha haki sawa (mirathi) kwa wanaume na wanawake<br><br>Boresha makazi ya kuishi kwa wananchi wengi wa Tanzania<br><br>Punguza maradhi yanayotokana na matumizi ya maji yasiyo salama katika maeneo ya mijini na vijijini | Ongeza uwezo wa watu katika maeneo ya vijijini na mijini kupata na kutumia vyanzo vya maji vya kuaminika na vya gharama nafuu, huduma za vyoo na huduma za maji taka. | Maji, mazingira | Maji na Maendeleo na Mifugo, Afya, Ujenzi, Tamisemi, Mamlaka za Serikali Za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kilimo na Uhakika wa Chakula, Ushirika na Masoko, Ofisi ya Makamu wa Rais, Tume ya Mazingira, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Sekta Binafsi, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | Fanya ukaguzi/uchunguzi kuhusu ubora wa maji na hakikisha kuwa vyanzo vya maji vinavyolindwa vilivyopo vinatunzwa vizuri na kufanyiwa matengenezo yanayohitajika. | Mazingira na maji | Tume ya Mazingira, Maji na Maendeleo ya Mifugo |
| | | Tekeleza hatua za usimamizi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira kama zinavyoainishwa katika Sheria inayoandaliwa ya Usimamizi wa mazingira. | Mazingira | Ofisi ya Makamu wa Rais, Tume ya Mazingira |
| | | Endesha programu na jenga ufahamu wa wananchi ili kupunguza uchafuzi wa hewa majumbani na kuendeleza matumizi ya majiko sanifu. (yanayotumia nishati kidogo) | Mazingira, jinsia | Tume ya Mazingira, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | Andaa na tekeleza mkakati wa kitaifa wa hifadhi ya jamii na ulinzi wa makundi watu walio katika hatari ya kuangukia katika umasikini (tekeleza Sera ya Hifadhi ya Jamii ya 2003) | Sekta mbalimbali | Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Fedha, TAMISEMI,Ofisi ya Makamu wa Rais, TASAF, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Sheria na Katiba, Jumuiya Huru za Kiraia, Sekta Binafsi |
| | | Boresha namna ya kushughulikia taka ngumu na maji taka, na hamasisha mbinu za kudumisha usafi wa kaya, hasa katika maeneo ya vijijini na makazi ya mijini. | Mazingira, Jinsia | Maji, Afya, Tume ya Mazingira, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | Boresha mifumo ya kuondoa maji ya mvua katika makazi duni na yasiyopimwa (unplanned) mijini. | Mazingira | Maji, Tume ya Mazingira, Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| | | Hakikisha kuwa kuna huduma ya kutosha ya vyoo katika taasisi zote za umma – shule, vituo vya afya, masoko na mahali pengine penye mikusanyiko ya watu. | Maji na usafi wa mazingira (maji taka) | Tume ya Mazingira, Maji, Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| | | Panua, karabati na jenga mifumo ya kuondoa maji taka, uzoaji takataka na hifadhi ya mazingira. | Mazingira | Ujenzi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maji na Maendeleo ya Mifugo |
| | | Weka msisitizo wa kipekee katika kushughulikia vikwazo vinavyowafanya wanawake na wajane wasiweze kupata mikopo. Wezesha upatikanaji wa nyumba bora na za gharama nafuu kwa kutoa mikopo na miradi ya kusaidiana (self help) ya ujenzi. | Makazi na jinsia | Ardhi, Fedha |
| | | Rekebisha maeneo ya makazi ambayo hayajapimwa na ongeza uzalishaji wa viwanja vilivyopimwa vikiwa na miundombinu muhimu. | Makazi | Ardhi |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au Maeneo ya Ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | | Boresha usimamizi wa ardhi na anza kutumia teknolojia za kuhifadhi maji, tekeleza mipango ya kitaifa ya kuzuia nchi kugeuka jangwa na uharibifu wa ardhi. | Mazingira | Kilimo, Tume ya Mazingira, Maji na Maendeleo ya Mifugo |
| | | Tekeleza sera za matumizi ya ardhi ili kukabiliana na maafa ya kimazingira (mfano, mafuriko na ukame) na weka taratibu za kushughulikia maafa hayo na athari zake pale yanapotokea. | Mazingira | Ardhi, Ofisi ya Waziri Mkuu |
| 4. Kutoa ulinzi wa kutosha kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuangukia kwenye umasikini (yaliyo katika mazingira magumu nk) na makundi yanayokosa mahitaji yao ya kimsingi na huduma | Watu walio katika hatari na hali ngumu zaidi ya kuangukia kwenye umasikini wanafikiwa na hatua thabiti za hifadhi na ulinzi wa jamii. (WKMVM)<br><br>Ongeza kiwango cha watu wenye ulemavu wanaoshiriki katika shughuli za kiuchumi hadi .......(WKMVM)<br><br>Punguza kiwango cha kaya masikini ambazo zina mzigo wa kuhudumia wazee, yatima, watoto walio katika mazingira magumu zaidi na watu wanaoisha na VVU/UKIMWI.<br><br>Ongezeko la 50% la utayari wa jamii kuwahudumia wazee hadi ifikapo mwaka 2010. | Fanya utafiti wa awali (baseline study) wa kupata takwimu za msingi zitakazotumika katika kuainisha malengo ya utekelezaji na kuweka shabaha sahihi ya kufikiwa ifikapo 2010. | Sekta mbalimbali | Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Afya, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Elimu na Utamaduni, Sheria na Katiba, Sekta Binafsi, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | Saidia kaya zilizoathirika na VVU/UKIMWI zinazoongozwa na vijana wa kike, watoto na wazee kwa kuwapatia misaada maalumu. | VVU/UKIMWI, jinsia, watoto na wazee | TACAIDS, Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya huru za kiraia, vikundi vya kijamii |
| | | Anzisha shughuli mbalimbali zenye kiwango cha juu cha ubora zinazolenga mahsusi kuwahudumia watu wenye ulemavu, watu wanaoisha na VVU/UKIMWI, watu wenye maradhi ya muda mrefu na wazee: shughuli hizo ni pamoja na kuwawezesha kupata huduma za jamii, mikopo; misamaha ya kuchangia gharama za huduma (cost-sharing); huduma za matibabu majumbani (home-based care), elimu na mafunzo ya ufundi stadi, uhamisho na pensheni. | Wazee, Ulemavu, utawala | Fedha, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Elimu na Utamaduni, |
| | | Tafiti mbinu au utaratibu wa kuweza kutoa hifadhi ya kijamii kwa kuwapa wazee kipato, kwa kupitia malipo ya pensheni ya kila mwezi ili kukidhi mahitaji yao muhimu. | Utawala | Fedha, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| | | Kuza na endeleza ushiriki wa wananchi katika ngazi ya jamii katika kubuni na kutekeleza hatua za mbalimbali za ulinzi na hifadhi ya jamii. | Utawala | Ofisi ya Makamu wa Rais, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| | | Tekeleza sera kuhusu hatari ya kuweza kuangukia kwenye umasikini (vulnerability) na hifadhi ya jamii, pamoja na taratibu zitakazowawezesha walengwa kupata misaada; sambaza taarifa kuhusu sera na taratibu hizo kwa walengwa wote. | Hatari ya kuwa masikini | Kazi na Maendeleo ya Vijana, Ofisi ya Makamu wa Rais, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| | | Panua, imarisha na endeleza miradi midogo midogo ya kijamii (micro and area based schemes), bima ya jamii na programu za utoaji misaada ya kijamii. | Hatari ya kuwa masikini, Utawala | Fedha, Kazi na Maendeleo ya Vijana |
| | | Imarisha uwezo wa mamlaka za serikali za mitaa kutambua watu masikini sana au wale walio katika hatari zaidi ya kuwa masikini na kuwapa msaada unaohitajika, ikiwa ni pamoja na kuwawezesha kupata huduma za serikali na kuboresha uwezo wa familia, jamii na taasisi za kijamii kuweza kukidhi mahitaji ya watu watu walio katika makundi haya. | Hatari ya kuwa masikini | TAMISEMI, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au Maeneo ya Ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | | Kuza na endeleza jitihada za sekta binafsi katika kutekeleza hatua za hifadhi ya jamii | Hatari ya kuwa masikini | Sekta Binafsi, Afya, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| 5. Weka taratibu zitakazohakikisha kuwa huduma bora za jamii zinapatikana kwa watu wote na kwa gharama nafuu | Boresha barabara za vijijini ili ziweze kupitika wakati wote kutoka 50% mwaka 2003 hadi angalau 75% mwaka 2010, (WU/TAMISEMI)<br><br>90% ya shule na 80% ya hospitali, zahanati na vituo vya afya katika maeneo ya mijini na vijijini zina mchanganyiko unaohitajika wa wafanyakazi wenye taaluma na hamasa ya kufanya kazi. (WEU/WA)<br><br>Wafanyakazi/wataalamu katika sekta ya jamii, miundombinu na utoaji huduma za kijamii wanahudhuria sehemu zao za kazi na kutekeleza majukumu yao kama inavyopasa.<br><br>Boresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wigo mpana zaidi. Kila kaya isiwe zaidi ya km. 5 kutoka kwenye kituo cha afya<br><br>Angalau 80% ya madawa muhimu yanapatikana wakati wote wa mwaka. Hii ni kwa kuzingatia mpango wa afya (health package) | Hakikisha kuwa miundombinu muhimu inakuwepo, hasa majengo na vifaa vya kutosha vya kutolea huduma na mtandao wa barabara zinazopitika, ili kuwezesha utoaji wa huduma za misingi za jamii. | Barabara | Fedha, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Elimu na Utamaduni, Afya, Ujenzi, Maji na Maendeleo ya Mifugo, Sekta Binafsi |
| | | Ongeza kiwango/kiasi halisi cha rasilimali zinazotumika moja kwa moja katika utoaji wa huduma za jamii. | Utawala | Fedha |
| | | Imarisha taratibu za rufaa katika ngazi ya wilaya ili kuwawezesha wagonjwa kupata huduma sahihi na za haraka katika ngazi za juu kama wanavyohitaji. | Afya | TAMISEMI, Elimu Na Utamaduni, Afya |
| | | Ongeza ufanisi na usawa katika matumizi ya fedha za umma hasa katika shughuli zinazowanufaisha masikini na wale walio katika hatari ya kuangikia kwenye umasikini. | Utawala | Fedha, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Elimu na Utamaduni, Afya |
| | | Hakikisha kuwa wafanyakazi wenye utaalamu na ari ya kazi wanaajiriwa haraka katika sekta ya huduma za jamii, wanapangiwa vituo vya kazi, wanapewa ujira wa haki na wanasimamiwa kikamilifu ili kuhakikisha utendaji mzuri na uwajibikaji. | Utawala | Fedha, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, TAMISEMI |
| | | Ondoa vikwazo vyote vinavyowafanya wananchi kutokupata huduma za afya kwa kutokuwa na ada ya matibabu kwa wagonjwa masikini, akina mama wajawazito na watoto na kuondoa ada za matibabu zisizo rasmi na kupunguza umbali kati ya wananchi na mahali wanapoweza kupata huduma za afya. | Afya | Afya, |
| | | Weka taratibu nzuri na zinazoeleweka za ugawaji wa dawa na mahitaji mengine katika ngazi za hospitali/vituo vya afya na wilaya ikiwa ni pamoja na kukidhi mahitaji ya mahali husika na mzigo wa maradhi: weka taratibu madhubuti za usambazaji na ukaguzi wa madawa (audit) kuhakikisha kuwa yanafika kule yanapohitajika. | Afya | Afya, TAMISEMI |
| | | Tekeleza na kamilisha mipango ya sasa ya kukarabati vituo vya afya, zahanati na hospitali ili kuongeza ubora wa huduma inayotolewa, hususan, katika ngazi ya huduma ya afya ya msingi. | Afya | Afya, TAMISEMI |
| | | Hamasisha na endeleza ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi katika kutoa huduma bora za jamii kwa gharama nafuu; msisitizo ukiwekwa katika kutoa huduma kwa masikini na makundi yaliyo katika hatari ya kuangukia kwenye umasikini. | Afya, elimu | Elimu na Utamaduni, Afya, Ujenzi, Maji Na Maendeleo Ya Mifugo, Sekta Binafsi |
| | | Hakikisha kuwa huduma muhimu za kijamii (maji safi na salama, umeme na vyanzo vingine vya nishati vya gharama nafuu, barabara na mifumo ya kuondoa maji taka) zinapatikana kwa kiwango cha kutosha katika maeneo ya mijini yasiyopimwa (unplanned) yaliopo hivi sasa na katika maeneo yaliyopimwa. | Utawala | Fedha, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Elimu na Utamaduni, Afya, Ujenzi, Maji Na Maendeleo Ya Mifugo, Sekta Binafsi |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au Maeneo ya Ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | Punguza idadi na kiwango cha kaya zinazoishi maeneo duni ya mijini yasiyopimwa (slums) na ongeza ukubwa wa maeneo yaliyopimwa yanayopatiwa huduma muhimu za kutosha(utilities) kama vile maji, umeme, simu nk | Weka mfumo wa kukusanya, kuchambua na kutumia takwimu kuhusu uwezo wa watu kupata kutumia na kunufaika na huduma mbalimbali (access) matumizi ya huduma hizo na matokeo yanayopatikana. Changanua (disaggregate) takwimu kwa hizo kwa jinsia, umri, hali ya kipato, eneo la kijiografia (na mambo mengine) ili kubainisha iwapo huduma hizo zinawafikia watu na kuwanufaisha kwa usawa. | Utawala | Fedha, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mipango Ubinafsishaji, Ofisi ya Taifa ya Takwimu |
| | Kuna ubia/ushirikiano mzuri na wa kiwango cha juu kati ya Jumuiya Huru ya Kiraia na sekta binafsi katika kupanua na kutoa huduma bora za kijamii. | Hakikisha kuwa mfumo wa ukusanyaji takwimu kutokana na utendaji wa siku hadi siku unawezesha kupatikana kwa takwimu thabiti, za kuaminika na zinazoweza kutumika katika kupanga vipaumbele, kubuni na kufuatilia mipango ya utoaji wa huduma za jamii. | Afya, elimu maji na utawala | Fedha, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Elimu na Utamaduni, Afya, Ujenzi, Sekta Binafsi |
| | Kuna mifumo mizuri inayoeleweka ya utayarishaji mipango na uchambuzi wa takwimu. | Oanisha (harmonise), punguza na rahisisha taratibu za utoaji taarifa na ukusanyaji takwimu ili ziweze kutumiwa kwa urahisi na watumiaji wa mwisho katika ngazi ya eneo au kituo. | Utawala | Fedha, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Elimu na Utamaduni, Afya, Ujenzi, Maji Na Maendeleo Ya Mifugo, Sekta Binafsi |


HUDUMA ZA JAMII
ASANTE KWA HUDUMA NZURI. KAMATA "CHAI" YAKO
TUTAFIKAJE?
Seri K. anasema...
HAYA YAMEPITWA NA WAKATI ... HUDUMA ZA JAMII ZITOLEWE KWA WOTE

## Eneo la 3: Utawala Bora na Uwajibikaji



# Eneo la 3: Utawala Bora na Uwajibikaji

**Matokeo Makuu Tarajiwa :**

1. Amani, utulivu wa kisiasa, umoja wa kitaifa na mshikamano vinaimarishwa na kuendelezwa.
2. Demokrasia na uvumilivu wa kisiasa na kijamii uanaimarishwa
3. Utawala bora na utawala wa sheria unakuwepo
4. Viongozi na watumishi wa umma wanawajibika ipasavyo kwa wananchi, kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupungua kwa rushwa na wananchi kuwa na uwezo wa kupata taarifa.

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| 1. Ulinzi binafsi umeboreshwa na vitendo vya uhalifu vimepungua. | Hakikisha kuwa taasisi na wakala wa serikali kama vile Jeshi la Polisi, Mahakama na Magereza wanazingatia kikamilifu haki za binadamu na kuhakikisha ulinzi na usalama wa wote. | ▪ Weka utaratibu ambao utawawezesha wananchi wote na hasa masikini na wale walio katika makundi yanayowekwa pembezoni umasikini kushughulikiwa matatizo yao kwa haraka na kwa haki katika mifumo ya polisi na magereza. | Sheria & makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikini | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, |
| | | • Ongeza uwezo wa jeshi la polisi kudhibiti kwa haki vitendo vya uhalifu na kushughulikia idadi kubwa ya kesi | Amani na Sheria/haki | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani. |
| | | • Punguza msongamano magerezani, tekeleza kikamilifu sera ya kutoa hukumu za kutumikia jamii (Community Sentencing Policy) na kusisitizia jukumu la mahakama la kurekebisha tabia kuliko kutoa adhabu. | Sheria/haki | Sheria na Mambo ya Katiba, Wizara ya Mambo ya Ndani. |
| | | • Shughulikia mahitaji maalumu ya ulinzi ya makundi yaliyo katika mazingira magumu, yanayowekwa pembezoni na yaliyo katika hatari ya kuangukia katika umasikini na yanayohitaji hatua tofauti za ulinzi. Makundi hayo ni pamoja na watoto, vijana (hususan wasichana) watu wenye ulemavu, watu wanaoishi na VVU/UKIMWI na wazee. | makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikini na jinsia | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Chukua hatua za kisheria na kiutawala za kuwalinda wanawake dhidi ya vitendo vya ukatili, kuelimisha na kujenga mwamko wa jamii kuhusu haki za wanawake ili wapate haki hizo, kuwalinda dhidi ya wale wanaokiuka haki hizo, na kuwa na taratibu za kuwashughulikia kisheria wakiukaji wa haki za wanawake | makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikini na jinsia | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Toa mafunzo ya haki za binadamu kwa polisi, magereza na vyombo vingine vya kusimamia utekelezaji wa sheria. Elimisha watu kuhusu haki zao za kikatiba na haki za binadamu | Haki za binadamu, Sheria, Jinsia | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia |
| 2) Kupungua kwa hali ya baadhi ya makundi katika jamii kutengwa (kuwekwa pembezoni) kisiasa na kijamii na kupungua kwa hali ya kutokuaminiana | Weka mifumo ya kisiasa na kijamii na taasisi zitakazowawezesha Ushiriki kamilifu wa wananchi wote na hasa masikini na wale wanaowekwa pembezoni. | • Buni na tekeleza kampeni za kuelimisha wananchi kuhusu haki zao na kushughulikia aina zote za ubaguzi na unyanyapaa. | Haki za binadamu Ushirikishaji Jamii | Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Afya, Elimu na Utamaduni, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais, Mipango Ubinafsishaji, Ofisi ya Waziri Mkuu, Jumuiya Huru za Kiraia |


| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | *Watu wanaowekwa pembezoni na hivyo kuwa katika hatari ya kuangukia katika umasikini ni pamoja na watoto, vijana, wanawake, watu wenye ulemavu, wazee, yatima na watu wanaoishi na VVU/UKIMWI* | • Pitisha sheria itakayowataka waajiri kutekeleza sera za kutoa fursa sawa ya ajira ambazo haziwabagui watu kwa misingi ya jinsia, umri, hali ya kuishi na VVU/UKIMWI, ulemavu au kuwa katika makundi yanayowekwa pembezoni (marginalised). | Jinsia, VVU, Ulemavu | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Jumuisha katika michakato ya mapitio muhimu (mfano, mapitio ya sekta za afya na elimu) uchambuzi wa kutengwa au kutokushirikishwa kwa watu walio katika makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuangukia kwenye umasikini. | Makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikini | Ofisi ya Makamu wa Rais, Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu Ofisi ya Rais - Mipango Ubinafsishaji, TAMISEMI, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Weka taratibu madhubuti na za kuaminika za watu hasa masikini na wale walio katika hatari zaidi ya kuangukia kwenye umasikini kutoa malalamiko yao na kuhakikisha kuwa wanalindwa dhidi vitisho au kuadhibiwa kutokana na kutoa malalamiko hayo. | Makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikini na jinsia | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Weka sheria na vifungu maalumu vitakavyoeleza wazi na kwa kina haki za watu wenye ulemavu na hatua zitakazochukuliwa pale ambapo haki hizo zitakiukwa. | Sheria na ulemavu | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia |
| 3. Miundo na Mifumo ya Utawala wa Kidemokrasia na utawala wa sheria ni ya uwakilishi, yenye uwajibikaji na inayowajumuisha kikamilifu wananchi. | Mifumo ya utawala iliyojengwa katika misingi ya uwakilishi, kujumuishwa kikamilifu kwa wananchi na uwajibikaji inakuwepo katika ngazi zote na kutekelezwa kikamilifu<br><br>Hakikisha kuwa vikao vyote vya kisheria vya jamii/serikali za mitaa vinafanyika kama ilivyopangwa (TAMISEMI). | • Panua na fuatilia utekelezaji wa Mwongozi wa Taifa kuhusu Utawala Bora | Utawala | Ofisi ya Rais - Mipango Ubinafsishaji, Fedha, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais – Ikulu, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Inua/boresha uwezo wa vyombo vyote vya uwakilishi, hususan, katika ngazi wilaya na vijiji ili viweze kutekeleza wajibu wake wa usimamizi | Kujenga uwezo | TAMISEMI,Ofisi ya Rais - Mipango Ubinafsishaji, |
| | | • Imarisha taasisi za utawala katika ngazi ya jamii (kupitia Programu ya kuboresha mfumo wa uendeshaji wa serikali za mitaa), ili wananchi wa kawaida waweze kushiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi, kubuni, kutekeleza na kufuatilia sera, taratibu na utoaji huduma. | Utawala shirikishi | Sheria na Mambo ya Katiba, TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Tekeleza na oanisha sera na sheria zinazohusu matumizi na usimamizi wa ardhi na maliasili, ikiwa ni pamoja na kutekeleza Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 na Sheria ya Vijiji ya mwaka 1992 na imarisha mahakama ya kutatua migogoro ya ardhi. | Mazingira | TAMISEMI, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Imarisha uhakika wa umiliki (tenure security) wa ardhi ya vijiji inayomilikiwa kwa pamoja (communally) au na mtu mmoja mmoja na ondoa vifungu vya sheria vinavyopingana vinavyosimamia sekta kama za madini na wanyamapori. | Mazingira | TAMISEMI, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Jumuiya Huru za Kiraia |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | | • Hakikisha kuwa kuna utaratibu utakaowawezesha wananchi kufuatilia na kuhakikisha kuwa watumishi na mamlaka mbalimbali za umma zinafikia viwango vinavyostahili vya maadili na uwajibikaji. | Uwajibikaji Utawala | Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, , Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Ongeza/panua ushiriki na uwakilishi wa wanawake, watoto, vijana, watu wenye ulemavu, watu wanaoishi na VVU/UKIMWI na makundi mengine yanayowekwa pembezoni, katika mifumo yote ya utawala. | Jinsia, watoto, vijana, Watu wanaoishi na VVU/ UKIMWI | Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Ingiza masuala ya jinsia (mainstream) katika sera, mipango, bajeti na katika taratibu zote za utekelezaji. Hii ni pamoja na kujumuisha viashiria vitakavyowezesha kufanyika kwa ufuatiliaji, uhakiki na uchambuzi wa kijinsia katika masuala ya utawala bora. | Jinsia | Ofisi ya Makamu wa Rais, Fedha , Ofisi ya Rais - Mipango Ubinafsishaji, Jumuiya Huru za Kiraia |
| 4. Haki za watu masikini na wale wanaowekwa pembezoni zinalindwa na kuimarishwa katika mfumo wa sheria | Hakikisha kuwa haki inatendeka kwa watu wote na kwa wakati, hasa kwa watu masikini na wale wanaowekwa pembezoni. | • Imarisha mfumo wa sheria katika ngazi zote, hasa katika ngazi ya mahakama za mwanzo ili kuongeza fursa ya watu kuzitumia, kuboresha uwakilishi wa wananchi, na kuboresha usikilizaji na utoaji hukumu katika kesi zinazowahusu watoto, vijana, walemavu, wazee na makundi mengine yanayowekwa pembezoni, | Sheria na makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikini na jinsia | Sheria na Mambo ya Katiba, Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, |
| | | • Endeleza na panua Programu ya Marekebisho katika Sekta ya Sheria huku msisitizo ukiwekwa katika kupunguza msongamano wa kesi ambazo bado hazijatolewa hukumu, kuboresha sheria ili ziweze kwenda na wakati (updating), kuimarisha usimamizi na mgawanyo wa majukumu kati ya vyombo na taasisi zinazosimamia sheria na usalama, kuimarisha uhuru wa taasisi za sheria na kuongeza kasi ya kushughulikia mashauri ya kisheria. | Sheria na kujenga uwezo | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani. |
| | | • Pitia sheria ya miradhi ili kutoa haki sawa kwa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana. | Jinsia | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya ndani, Maendeleo ya Jamii , Jinsia na watoto, Jumuiya huru za kiraia |
| | | • Ongeza uwezo na mahakama wa kushughulikia idadi kubwa ya kesi kwa haki na ufanisi zaidi. | Sheria | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani. |
| | | • Imarisha ufuatiliaji wa mfumo wa sheria kwa kuhakikisha kuwa kuna taratibu ambazo wananchi wanaweza kufuata iwapo hawakuridhika na maamuzi yaliyofanyika, (taratibu za kutoa na kushughulikia malalamiko ndani ya mfumo wa sheria na katika mifumo ya polisi na magereza); hakikisha upatikanaji wa takwimu za kuaminika kuhusu matukio ya uhalifu yaliyoripotiwa, watu walio kizuizini, kesi zilizo mahakamani, malalamiko n.k. ambazo zinaweza kulinganishwa baina ya wilaya. | | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani. |
| | | • Anzisha mfumo wa kushughulikia masuala ya kisheria yanayohusu watoto –kuwa na mahakama za watoto zenye kuzingatia haki na maslahi ya mtoto kama msingi mkuu wa shughuli zake zote. | Sheria na watoto | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani. |
| | | • Tokomeza aina zote za ubaguzi dhidi ya watoto, vijana, watu wenye ulemavu, wazee, watu wanaoishi na VVU/UKIMWI na makundi mengine yaliyo katika hatari ya kuangukia katika umasikini. | Sheria, sera na makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikini | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Boresha vitendea kazi, miundombinu na utendaji wa polisi, magereza na mahakama ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na bila kujiingiza katika vitendo vya rushwa. | Sheria | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani. |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| 5. Mgawanyo sawa wa rasilimali za umma na suala la rushwa limeshughulikiwa kikamilifu | Rasilimali za umma zimegawanywa na kutumiwa katika misingi ya usawa, uwajibikaji na uwazi. | • Jumuisha kipengele kuhusu usawa na kushirikishwa kwa wananchi katika Mapitio ya Matumizi ya Serikali (PERs) na katika tafiti za kufuatilia matumizi ili kuona iwapo bajeti, fedha zilizotolewa na matumizi ya fedha hizo zina muelekeo wa kuwasaidia masikini (Pro-poor), hususan, katika kushughulikia mahitaji ya masikini na makundi ya watu walio katika hatari ya kuangukia katika umasikini (mfano, watoto, wanawake, wazee, watu wenye ulemavu nk.) | Jinsia na makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikini na jinsia | Fedha, Ofisi ya Rais - Mipango Ubinafsishaji, Ofisi ya Makamu wa Rais, Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | | • Weka taratibu nzuri za kuhakikisha watu masikini na wale walio katika makundi yalio katika hatari ya kuwa masikini wakuwa na fursa sawa ya kupata huduma za jamii; waelimishe wananchi kuhusu sera za serikali kuhusu ugharimiaji wa huduma za umma na ada rasmi pamoja na haki zao kwa kuwapatia elimu ya uraia na taarifa. | Jinsia, makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikini, utawala | Ofisi ya Rais – Ikulu. Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia, Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani |
| | | • Imarisha mifumo na taasisi za kuhakikisha uwajibikaji, uadilifu, na uwazi wa viongozi wa serikali na wa mashirika yasiyo ya kiserikali ikiwemo vyama vya siasa. | Utawala, uwajibikaji | Ofisi ya Rais – Ikulu. Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | | • Imarisha, endeleza na fuatilia vigezo na utaratibu unaotumika (formula) katika mgawanyo wa rasilimali. | Fedha, utawala | Fedha, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais-Mipango na Ubinafsishaji. |
| | | • Toa usimamizi wa kutosha kwa Halmashauri za Wilaya ili kuwezesha/kukamilisha uwekaji wa kumbukumbu zao za mahesabu, utoaji wa taarifa za fedha na ukaguzi | Fedha, utawala | Fedha, TAMISEMI |
| | | • Ongeza ushiriki wa wananchi katika kutayarisha, kubuni na kufuatilia Mkakati wa Kupunguza Umasikini, Mapitio ya Matumizi ya Serikali na Bajeti, ikiwa ni pamoja na kusambaza taarifa kuhusu bajeti, mapato na matumizi hadi katika ngazi ya jamii. | Ushirikishaji na utawala | Fedha, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais – Mipango na Ubinafsishaji, , Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | | • Imarisha uwezo wa Halmashauri za Wilaya, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali katika kusimamia rasilimali na mamlaka yao. | Jenga uwezo | Fedha, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais – Mipango na Ubinafsishaji, |
| | | • Weka taratibu za kisheria za kuziwajibisha halmashauri, , Idara, Wakala wa Serikali na Wizara zinazoshindwa mara kwa mara kupata hati ya kuwa na mahesabu mazuri na halisi ya mapato na matumizi yao (clean certificate) wakati wa ukaguzi wa vitabu vyao vya mahesabu. | Fedha, utawala | Fedha, TAMISEMI |
| | | • Hamasisha na wezesha wadau (ikiwa ni pamoja na jamii zenyewe) kuchangia katika kuboresha ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma kwa kupitia ukusanyaji, uchambuzi na matumizi ya takwimu. | Utawala shirikishi | Ofisi ya Rais – Mipango na Ubinafsishaji, TAMISEMI, Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | Weka taratibu, kanuni na miongozo kuhusu namna ya | • Imarisha mifumo na vyombo vilivyopo (Mfano TAKURU) ili viweze kufanya kazi zake kwa uhuru na kuweza kuchukua hatua kali dhidi ya rushwa ndogo na kubwa. | Utawala, rushwa | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani. |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | kukabiliana na rushwa ndogo na kubwa, | • Imarisha na tekeleza sheria kuhusu rushwa ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa na Mpango wa Utekelezaji wa Kukabiliana na Rushwa na kuhakikisha kuwa Wizara, Idara na Wakala wote wa serikali wanakuwa na mipango yao mahsusi ya kupunguza na kufuatilia suala la rushwa katika sekta zao. Kuziwajibisha Wizara, Idara na Wakala hao ili waweze kusimamia na kushughulikia suala la rushwa kikamilifu. | Sheria, Utawala na rushwa | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Ofisi ya Rais-Ikulu, Ofisi ya Waziri Mkuu. |
| | | • Kuwa na takwimu za kutosha zinazoweza kulinganishwa (comparable) ili kuwezesha ufuatiliaji wa kudumu viwango vya uwajibikaji kuhusu masuala ya fedha katika ngazi ya wilaya, ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa mahesabu ya mamlaka za serikali za mtaa. | Utawala na uwajibikaji | Fedha, TAMISEMI, Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | | • Weka taratibu za kubaini, kuchunguza na kufungua mashtaka ya ubadhilifu wa fedha za umma, rushwa ndogo na kubwa. | Sheria, Utawala na rushwa | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Ofisi ya Rais-Ikulu, Ofisi ya Waziri Mkuu , Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | | • Imarisha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu kutokana na utendaji wa kazi za siku hadi siku ili kupima kiwango, ukubwa na aina ya umasikini na sababu zinazowaweka watu katika hatari zaidi ya kuwa masikini, kwa ajili ya kutumiwa katika kuandaa sera, kutenga rasilimali, kuamua shughuli za kufanya nk. Hakikisha kuwa takwimu hizo zinasambazwa kwa wananchi kwa kiwango kikubwa kwa kupitia Internet na njia nyingine za mawasiliano zitakazoweza kufikisha ujumbe kwa wa urahisi kwa jamii. | Utawala | Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais – Mipango na Ubinafsishaji, Fedha, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Weka wazi kwa jamii na wawezeshe kupata sheria, sera na fedha zinazotengwa na kutolewa kwa ajili ya makundi yaliyo katika hatari za kuangukia katika umasikini kwa ajili ya taarifa na matumizi yao. | Utawala na makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuwa masikin | Sheria na Mambo ya Katiba, Mambo ya Ndani, Ofisi ya Rais-Ikulu, Ofisi ya Waziri Mkuu , Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | | • Weka utaratibu wa kutangaza mara kwa mara hadi katika ngazi ya jamii au taasisi husika, mgawanyo wa fedha baada ya bajeti, utoaji wa fedha hizo (disbursements) na matumizi yake, mfano kwa kupitia mbao za matangazo za vijiji na mbao za matangazo kuhusu usimamizi wa fedha katika ngazi ya wilaya. | Fedha, utawala | Fedha, TAMISEMI, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Ongeza ushiriki wa jumuiya huru za kiraia katika ngazi zote katika michakato ya utayarishaji sera ikiwa ni pamoja na kuweka mipango na ufuatiliaji. | Utawala shirikishi | Ofisi ya Makamu wa Rais, TAMISEMI, Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Jumuiya Huru za Kiraia |
| | | • Linda na endeleza uhuru na uwezo wa vyombo vya habari | Utawala | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| 5. Kuna muundo mzuri wa utumishi wa umma ili kweka msingi wa kuboresha utoaji wa huduma za jamii na kuondoa umasikini. | Mifumo ya utawala wa serikali inaendeshwa kwa uwazi na kwa maslahi ya watu inaowahudumia (ORMUU) | • Imarisha na tekeleza Programu ya Uboreshaji Utendaji katika Utumishi wa Umma msisitizo ukiwekwa katika kuwa na taratibu za uajiri zenye uwazi zinazozingatia sifa, tabia, maadili, ujuzi na uwezo wa mtumishi, maadili, sheria na motisha ya kada husika, usimamizi wa kitaasisi, kuzingatia matumizi mazuri ya fedha/rasilimali yenye ufanisi na yanayolingana na matokeo (cost effectiveness), huduma bora kwa wateja na kujali na kushughulikia matatizo ya wananchi (responsiveness). | Utawala | TAMISEMI, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, |

| Malengo | Matokeo ya Kiutendaji | Mikakati ya eneo hili | Sekta au maeneo ya ushirikiano | Wahusika/Sekta |
|---|---|---|---|---|
| | | • Fanya tafiti za mara kwa mara kuhusu utoaji wa huduma za jamii na kiwango cha wateja kuridhishwa na huduma zinazotolewa ili kufuatilia ubora wa huduma na kusambaza matokeo ya utafiti huo kwa wadau wote kwa mujibu wa misingi ya utawala bora. Ongeza njia ambazo wateja wanaweza kuwawajibisha watoa huduma. | Uwajibikaji na utawala | Ofisi ya Rais – Ikulu. Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | | • Imarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kuwa viashiria vya utendaji vinaweza kuhakikiwa/kutathminiwa kwa kulinganisha na malengo na shabaha ya kila wizara, idara na wakala wa serikali. | Utawala | Ofisi ya Rais – Mipango Ubinafsishaji, Ofisi ya Makamu wa Rais, Fedha, UNDP, TAMISEMI |
| | | • Anzisha, tekeleza na fuatilia maoni ya wananchi (feedback) kuhusu Mikataba ya Huduma kwa Wateja (client service charters) pamoja na tafiti kuhusu watumiaji wa huduma (end-users) katika kila sekta. | utawala | Ofisi ya Rais – Mipango Ubinafsishaji, Ofisi ya Makamu wa Rais, Fedha, TAMISEMI, Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | | • Anzisha mbinu nzuri za kibunifu za kuwasaidia na kuwasimamia wafanyakazi wanaotoa huduma za jamii zitakazowawezesha kutambua kero muhimu za wananchi na kuboresha utoaji wa huduma. Endeleza ubia kati ya serikali, sekta binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali katika utoaji wa huduma. | Mifumo ya utawala | Ofisi ya Rais – Ikulu. Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Jumuiya Huru za Kiraia. |
| | | • Ajiri haraka wafanyakazi wenye sifa katika sekta muhimu ambao wana elimu na hamasa/moyo wa kazi. Wapangie wafanyakazi hao katika vituo vya kazi kwa usawa na wasimamie. | Kujenga uwezo | Ofisi ya Rais – Ikulu. Menejimenti ya Utumishi wa Umma. |
| | | • Ongeza na rekebisha (ili kuweka vigezo vya haki) mishahara na marupurupu ya wafanyakazi wa serikali ili kuwapa ujira wa haki kwa kazi wanazozifanya na kupunguza rushwa. | Kujenga uwezo, rushwa | Ofisi ya Rais – Ikulu. Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. |



HUPITI!
HATUTAKI MASWALI
TAKRIMA
BAKSHISHI
RUSHWA
1000/=
100
ASANTE
ZAWADI
CHAI
50
Seri K. anasema...
HAYA YAMEPITWA NA WAKATI...SASA TUNATAKA UWAZI NA UWAJIBIKAJI